# *Sisi Tunataka Kumwona Yesu*

Asante, Ndugu Roy. Mwaweza kuketi. Hakika ninahesabu haya kuwa majaliwa makuu kuwa hapa katika jiji hili la kupendeza, usiku wa leo, pamoja nanyi Wakristo, ambao ni wasafiri na wageni kwa dunia hii. Nasi tunakiri kwamba tunautafuta Mji ambao...ambao Mbuni na Mjenzi wake ni Mungu, tukidai kuwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu; walio ndani ya Kristo ni Uzao wa Ibrahimu na ni warithi pamoja naye sawasawa na ahadi.

2 Tunawaletea salamu kutoka kwa Wakristo wengine ulimwenguni kote, nami nina hakika ya kwamba wangependa kuwa hapa, sisi sote pamoja, usiku wa leo, kwa ajili ya ibada ya kuabudu, lakini tunautazamia wakati ambapo tutakuwa pamoja, kwa Ibada ya kuabudu tutakapomvika taji kuwa Mfalme wa mfalme na Bwana wa mabwana.

3 Sisi ni...Nilikuwa tu nikielewa kwamba tulifika hapa, kwenye wakati huu tu, wakati madhehebu kadhaa yanao, ninaamini, mkutano mkubwa. Nasikitika kwamba tulifika wakati huo, maana najua jinsi mnavyojisikia, ninajua jinsi ndugu wanavyojisikia kuwa...jambo kama hili kutukia, kwenye wakati tu ambapo wana mkutano wao mkubwa. Na Ndugu Eddie Byskal, ndugu na rafiki yangu, ndio wakati pekee tungeweza kuwa hapa, tukipita tu, na hiyo ndiyo sababu walifanya haraka sana, ibada tatu tu, kisha tunaendelea na safari. Nasi tunatumai kwamba Mungu atatujalia baraka kubwa kwa kukusanyika kwetu pamoja, na tunatumaini ya kwamba watakuwa na mojawapo ya mikutano mikubwa sana ya kambi, ama mikutano mikubwa, ama chochote walicho nacho, ambayo wamekuwa nayo kwa miaka mingi, tukitumaini kwamba Mungu atakuwa pamoja nao na kuwasaidia.

4 Sasa, ni vizuri kutembeleana, na kuwaona watoto wote wa Bwana. Nimekuwa...Sijawahi kuwa humu kisiwani hapo kabla. Tumeondoka hivi punde tu huko Port Alberni, na huko, ambako tulikutana na marafiki zetu Wahindi na wengi wa wazungu, nasi tulikuwa na mkutano mzuri sana siku tatu usiku pamoja nao. Nilikusudiwa kuwa hapa msimu uliopita wa kuchipuka, wala nisingeweza kuja wakati huo, kwa sababu ya mlipuko wa bunduki ambayo nilikuwa nikilenga shabaha. Nami nilikuwa nimechukua bunduki ambayo haikuwa imetobolewa vizuri, nayo ikalipuka moja kwa moja usoni mwangu, na nusura inipofushe kwa siku chache na kiziwi, na mbaya sana.

Ilipaswa, kulingana na jinsi ilivyopaswa kuwa, ilionekana kana kwamba, ingeulipulia mbali mwili wangu wote, kutoka kiunoni mwangu. Ilikuwa kama pauni elfu moja mia sita na themanini za shinikizo, zilizorudi moja kwa moja, pamoja na bunduki nzima na kadhalika, usoni mwangu, na darubini, na hata haikunikwaruza. Kwa hiyo na—nashukuru kwa hilo. Lakini kamwe nisingeweza kuona, na kwa namna fulani ilikuwa ni vigumu kusikia kwa siku chache, kama mlio wa kengele.

5 Nami nilipaswa kuondoka yapata siku moja kabla, basi tuliupangia tu mkutano kwenye wakati huu, na ndio wakati pekee ningeweza kupatikana, kwa sababu tulipaswa kuwa papa hapa Washington, na hiyo ndiyo sababu tumekuja. Na kama kuna mtu yeyote hapa kutoka kwa viongozi wa mikutano hi-, . . . mkutano huu mkubwa unaoendelea, waambieni kwamba sikufanya hivi makusudi, kwa sababu walikuwa na huu mkutano mkubwa, nilifanya hivyo tu, kwa sababu nilipitia. Na baadhi ya watu ambao hawakuweza kuhudhuria huo mkutano, ama mkutano wa kambi, chochote kile, mbona, wanaweza kupitia hapa, tupate wakati mdogo wa ushirika pamoja nao. Walikuwa na ratiba yao, bila shaka, tayari imewekwa, au labda ningeweza kwenda kambini, au chochote kilichokuwa na kusema nao, lakini wao . . . Ingenilazimu kuwafahamisha mapema, kwa sababu wame—wameweka ratiba yao, na bila shaka nisingependa kuingia wakati mtu mwingine . . . na kuchukua nafasi ya mtu mwingine. Na kuna . . .

6 Tuko hapa kuwaombea wagonjwa, na kuomba pamoja na waliopotea, kama kuna yeyote anayekuja kuombewa, tungefurahi kufanya hivyo, na kushiriki tu katika Neno. Ninapenda hilo, kuwa na ushirika katika Neno la Mungu. Sasa, ikiwa unamjua mgonjwa yeyote ambaye hahudhurii hiyo kambi au mkutano mkubwa, vema, shika simu asubuhi na kuwapigia simu, hebu tuwalete wote hapa na kuwaombea, na labda huenda Bwana akawaponya. Ninaamini Yeye atawaponya.

7 Sasa, nafikiri Ukristo unashawishi, nao ni . . . kama ukihubiriwa katika urahisi wake naye Mungu ataudhihirisha Ukristo katika Uwepo ulio Hai. Sasa, ikifikia tu kwenye desturi za dini, kanuni za imani, hazishawishi sana, kwa sababu zi—zinaeleweka vibaya mno, ni . . . zina kasoro. Hapo ni wakati ambapo mwanadamu ameuchafua kwa kuongezea fundisho la sharti na kadhalika kwake, ndipo haushawishi hata kidogo. Lakini kuona tu Biblia dhahiri ikisomwa tu, na kuiona ikitenda kazi na kuishiwa miongoni mwa watu, nafikiri inashangaza sana, mimi mwenyewe, na—naupenda sana. Na labda . . .

8 Mimi—mimi ni mtu wa kusini, na kila mtu, tangu nimekuwa hapa, wananiambia ninazungumza kigeni. Natumai sizungumzi kigeni kwenu, kwa sababu nilijaribu kuachana nayo, kadiri nilivyoweza, kujaribu kuongea kama ninyi Wakanada, lakini si—sinayo kabisa ndani yangu, si—si—siwezi kufanya hivyo

kabisa. Na, ili kwamba, ninatumaini ya kwamba Roho Mtakatifu atawafunulia kile ninachojaribu kuwaletea, ma—maneno yangu.

9 Na sasa, tunaamini kwamba ni . . . kwamba Ukristo unashawishi, na ndipo tunakuja, si tukiwakilisha dhehebu lolote, bali tukiyawakilisha yote. Na njia ya . . . Tunaamini kwamba Kristo ndiye Kichwa cha Kanisa, ambalo amenunua kwa Damu Yake Mwenyewe, na "kwa Roho mmoja, sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Tu—tunaamini ya kwamba tunajiunga na madhehebu yetu mbalimbali, bali tunabatizwa kuwa Mwili mmoja, Kristo, kwa Roho Mtakatifu, Bwana mmoja, imani moja, na ubatizo mmoja. Sikuzote nimetoa tamshi dogo, loo, si kila wakati, bali mara nyingi, nikisema, "Mwajua, nimekuwa wa familia ya Branham kwa miaka hamsini na mitatu, na kamwe hawakuwahi kuniomba nijiunge na hiyo familia. Nilizaliwa Branham." Na hivyo ndivyo ninavyowazia kwamba sisi ni Wakristo. Tumezaliwa Wakristo.

10 Sasa, tuna madhehebu yetu. Na mara nyingi, loo, Methodisti, Presbiteri, Katoliki, Anglikana, na kadhalika, hujaribu kusema ya kwamba sisi ni dhehebu la Kipentekoste. Hilo ni kosa. Sisi . . . Huwezi kuundia Pentekoste dhehebu, Pentekoste ni tukio kwa waaminio wote. Mnaona? Ni tukio. Nina marafiki wengi wa Anglikana ambao wana Roho Mtakatifu. Nina Wamethodisti wengi . . . Ndio kwanza nisaidie kuwaongoza Walutheri mia nne kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mnaona? Na kwa hivyo, kuna Chuo kizima cha Bethania kilichompokea Roho Mtakatifu kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, mnaona, si—si ninii—si dhe—dhehebu, ni tukio kwa yeyote atakaye.

11 Katika Afrika miongoni mwa makafiri na Wahotentoti, niliona wenyeji elfu thelathini wavaao blanketi wakimpokea kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, mnaona, huko India, ambako tulikuwa huko Bombay, na kusanyiko kubwa zaidi nililopata kuzungumzia maishani mwangu, kwenye kusanyiko moja, loo, karibu nusu milioni, nadhani, lakini niliona maelfu mara maelfu yao, wasiohesabika, ambao hata sikuweza kuona kulikuwa na wangapi, wakimkubali Kristo kama Mwokozi kwa wakati mmoja. Nao ni wa . . . Walikuwa Waislamu, Mabaniani, Wabudha, Makalasinga, Wajaini, na wengineo. Mnaona? Lakini wo—wote waliipokea Pentekoste, mnaona, kwa sababu ni kwa ajili ya "yeyote atakaye," anaweza kuwa mshiriki Wake. Naye Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Naye ajaye, bila shaka, ana Uzima wa Milele pamoja na hakikisho la kufufuliwa tena katika siku ya mwisho.

12 Kwa hivyo, ni hakikisho na raha iliyoje kuwa Mkristo, kujua kwamba katika siku hii, wakati ulimwengu una wasiwasi sana . . . Sasa, sijui watu wa Kanada wanajisikiaje sasa, lakini Wamarekani wanaweka udanganyifu mkubwa sana kuliko wote niliowahi kuona, kama vile tu karibu sehemu zote za ulimwengu.

Wanajifanya hawaogopi, lakini wanaogopa kabisa. Wanaificha serikali mahali pa kila namna, na kuchimba chini ardhini. Inanikumbusha juu ya mvulana mdogo akipitia kaburini usiku, akipiga mbinja, akisema yeye ni jasiri sana. Anapiga tu mbinja gizani. Matendo yao yanazungumza kwa sauti kubwa kuliko maneno, kwa sababu wakati umewadia ambapo hatutahitaji tena vikosi vya majeshi, ni shabiki mmoja tu afyatue kombora, dunia nzima italipuliwa. Siamini itatokea, Mungu hawezi kulishinda kusudi Lake Mwenyewe. Dunia iliwekwa hapa, na kutakuwa na utawala wa miaka elfu moja juu ya dunia, kwa miaka elfu moja, baada ya Kanisa kupelekwa Nyumbani. Kwa hivyo dunia haitalipuliwa, kwa hivyo iweni tu na hakika kwamba halitatokea, ni udanganyifu tu.

13 "Ndipo wakati mambo haya yanapoanza kutimia, basi tuinue vichwa vyetu; ukombozi unakaribia." Usiangalie chini na kuchoka, tunafika tu mahali pa kule Kuja kwa Bwana wetu Yesu. Badala ya kuchoka, tunapaswa kuwa watu wenye furaha zaidi ulimwenguni kote, na ndivyo tulivyo, bila shaka, tuko hivyo, kwa sababu hatuogopi mabomu. Mbona, mabomu hayatusumbui.

14 Na kama nilivyosema hivi majuzi usiku, huwezi kuchimba chini vya kutosha kuikwepa. Mbona, hatukufanywa fuko, tuliumbwa kuishi juu, dunia. Mnaona? Kuishi kwa amani na upendo, tukimtumaini Mungu. Nao wanajaribu kujenga makimbilio ya kujisetiri na mabomu na kuyajenga kwa feleji. Mbona, kama ungechimba futi milioni moja chini ya ardhi, mbona, ungali utapotea mara tu hilo bomu likipiga. Likipiga popote ndani ya maili mia moja, au maili mia mbili kutoka ulipo, mbona, mtikisiko huo ungevunja kila mfupa katika mwili wako huko chini. Litalipua shimo lenye kina cha yadi mia moja na hamsini, na kwa maili mia moja na hamsini mraba, na hayo ni yale wanatufahamisha. Hatujui waliyo nayo ambayo hawajatufahamisha.

15 Lakini mnajua, kuna jambo moja zuri, mnajua, sayansi inaweza kusuluhisha kila aina ya mambo, lakini Mungu yuko mbele sana kuliko hayo, tuna kimbilio la kujisetiri na mabomu, halijatengenezwa kwa feleji, limetengenezwa kwa manyoya, chini ya mbawa Zake, tunapumzika. Mara tu litakapolipuka . . . kabla halijalipuka, tutakuwa tumeondoka, tukaingia kwenye Nchi, ambako hakuna magonjwa, huzuni, ambako uzee utafanywa upya uurudie ujana, na Huko tuwe hivyo milele. Je, hiyo si ni faraja kwetu, hasa sana, sisi wazee? Vijana . . . Lakini kumbukeni tu, ni hivi karibuni sana.

16 Nilikuwa nikizungumza kwenye chama cha Kiwanis hapa si muda mrefu uliopita, na kulikuwa na daktari mmoja mzuri, madaktari kadhaa walikuwepo na walikuwa wakiniuliza kuhusu maisha ya misheni na kadhalika, ndipo daktari mmoja mzuri, alionekana mtu mzuri, lakini kamwe hakuweza kuamini

hilo, juu ya kuzaliwa na bikira, naye akasema tu asingeweza kuamini kuwa Mungu yupo.

17 Nami nikasema, “Sitaki kamwe uniguse kwa kisu cha upasuaji. Ningehofu kukuamini, Daktari, kama hukumwamini Mungu.” Na kwa hiyo mtaalamu mwingine alikuwa amesimama karibu nami, ambaye alikuwa mwaminio shupavu.

Naye akasema, “Vema, nafikiri chochote ambacho hakijathibitishwa kisayansi si halisi, Bw. Branham.” Akasema, “Ninaamini katika sayansi.”

18 Nikasema, “Nami pia, ninaamini unaweza kupanda mti wa sayansi mpaka ufikie mwisho wake, kisha uhamie kwenye mti wa imani na kuendelea tu kupanda,” nikasema, “kwa sababu ni. . .ninaamini katika kupanda juu ya mti.”

Akasema, “Vema, chochote ambacho hakiwezi kuthibitishwa kisayansi si halisi.”

“Loo,” nikasema, “Daktari, hilo ni tamshi baya sana kwako kutoa.”

Naye akasema, “Kwa nini hivyo?”

Nikasema, “Nitachukua kinyume chake: Chochote kinachoweza kuthibitishwa kisayansi si halisi.”

“Loo,” akasema, “unaongea, Ndugu Branham, kana kwamba umevurugwa.”

19 “Vema,” nikasema, “unaposema hakuna Mungu yeyote, unaongea kama asiyewajibika. Kwa hiyo, ‘Mpumbavu amesema moyoni mwake, “Hakuna Mungu.”’” Kwa hiyo tukaanza kuongea dhahiri sana mmoja kwa mwingine, nami nikasema, “Sasa, angalia, daktari. Je, wewe ni mtu aliyeoa?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Unampenda mke wako?”

Akasema, “Kama sikumpenda, nisingemwoa.”

“Je, una watoto?”

“Naam.”

Nikasema, “Basi kuna tofauti gani ya upendo, ulio nao kwa mke wako, kuliko ule ungekuwa nao kwa mwanamke mwingine yeyote?”

“Loo,” akasema, “kwa sababu yeye ni mke wangu, watoto wangu. . .mama wa watoto wangu.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.” Mnaona? Nilimshika papo hapo kwa hila yake basi. Nikasema, “Ati ulisema nini? Ulimpenda?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Unajuaje kwamba unampenda?”

Akasema, “Naam, bila shaka, najua ninampenda.”

20 Nikasema, "Sawa basi, upendo ni nini? Nionyeshe kisayansi. Hebu tushuke twende kwenye duka la dawa, nawe unidunge ratili moja yake, ndani ya mishipa yangu, ninauhitaji."

21 Basi, kulingana naye, hakuna kitu kama upendo kwa sababu huwezi kuthibitisha kisayansi ni kipi ndani yako ambacho ni upendo. Silaha zote za Kikristo ni imani, isiyoonekana. Mnaona? Silaha za Kikristo ni nini? Upendo, furaha, amani, imani, uvumilivu, upole, unyenyekevu, subira, Roho Mtakatifu, Mungu, Malaika. Zote ni za kimbinguni. Na kila kitu cha asili kimetoka ardhini na kitarudi ardhini. Mambo ya kimbinguni tu ndiyo yanayoishi, ndiyo ya Milele.

Nilikuwa na kitu kidogo kwake. Nikasema, "Daktari, nitakuuliza swali. Je, unaamini kwamba mwanadamu aliumbwa kutokana na mavumbi ya ardhi?"

22 Akasema, "Loo, ni—ningeweza . . . Ninaamini kwamba mwanadamu ni mavumbi ya ardhini. Naam, bwana." Kasema, "Je, unaona . . . Unakula chakula, nacho chakula kinageuka kuwa . . . kuwa damu, nayo damu inajenga tishu. Na kwa hiyo, inakuja . . . Unakula ninii . . . kama vile unavyokula nyama, na kadhalika, nayo hutengeneza kalisi, potashi, na chochote kile, chuma, na . . . unachohitaji kwa ajili ya mwili wako, nayo inakijenga."

23 Nikasema, "Kwa hiyo, labda kwa njia nyingine, unaamini kwamba mwanadamu alitoka katika mavumbi ya ardhi, lakini Mungu, hapo mwanzo, hakumwumba mwanadamu asili ambaye sisi ni mazao yake."

Naye akasema, "Labda hivyo ndivyo ungelielezea."

24 Kwa hiyo nikasema, "Ningependa kukuuliza, swali." Nami nikasema, "Sasa, tutasema jambo fulani hapa. Nitaninii . . . Je, ni kweli kwamba nimeumbwa na elementi kumi na sita (Ulikubaliana na hilo.) . . . "

"Naam."

25 " . . . za ardhini? Sasa basi, nilipokuwa na umri wa miaka kumi na mitano, nilikuwa mvulana mdogo, mwenye nguvu na hodari. Na sasa, kila ninapokula, unasema mimi . . . hicho chakula kinatengeneza seli za damu."

Kasema, "Hiyo ni kweli."

26 Nikasema, "Basi kila nilapo ninafanya upya maisha yangu." Hiyo ni kweli. Damu ni uhai, uhai ni damu, hakika. Mnaona? "Kila ninapokula ninafanya upya maisha yangu."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

27 Nikasema, "Basi maadamu ninakula, kwa nini nife? Unaona? Maadamu unaweza kujaza chakula humo, kwa nini nife? Mnaona, mimi huishi kwa seli za damu ninazoishia, nacho chakula hutengeneza seli za damu. Ndipo basi, kama—kama

nikiyafanya upya maisha yangu...” Nikasema, “Hili hapa jambo lingine ningependa kukuuliza. Nilipokuwa na miaka kumi na sita, nilikula chakula kile kile ninachokula sasa hivi, ila sasa ninakula kingi na bora zaidi. Na nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, kumi na mitano, kumi na sita, kila nilipokula nilizidi kuwa mkubwa na mwenye nguvu. Kisha kwa ghafla nilipofikia, yapata, takriban miaka ishirini na mmoja, kutoka hapo hadi karibu ishirini na mitatu, nikadumaa. Sasa, mimi nina hamsini. Ninakula chakula kile kile nilichokula wakati huo, basi ni kwa nini ninazidi kuwa dhaifu wakati wote, badala ya kukua, ninapokula chakula kile kile, nikiweka aina ile ile ya uhai ndani yangu?” Hilo hapo moja kwa ajili yako.

28 Hapa, kama nina jagi mkononi mwangu, au gudulia, nikimimina maji kwenye bilauri, na kumimina maji kutoka kwenye jagi hili kubwa, lililojaa, au bilauri, au gudulia ndani ya bilauri, na ijae nusu, na kisha niyamimine haraka zaidi, na kadiri ninavyoyamimina, ndivyo yanavyozidi kupungua. Nithibitishieni kisayansi imekuwaje kwa hiyo bilauri ya maji. Hakuna jibu kwa hilo. Mnaona?

29 Naam, hicho ni kitu kile kile. Niliweka chakula mwilini mwangu nikiwa na miaka kumi na sita, nikiwa na umri wa mwaka mmoja hadi kumi na sita. Nilipozaliwa, nilianza kula chakula cha ardhini, nami nikaanza kupata nguvu zaidi na zaidi, na mkubwa zaidi, nikiwa mtu mkubwa zaidi wakati wote, na kwa ghafla ikakoma. Namimina ndani chakula kile kile, unaendelea kupungua *hivi*, wakati nilipokuwa nikimimina chakula ndani nikipanda namna *hii*. Mnaona? Hakuna jibu kwa hilo, rafiki. Mungu ameweka miadi, na hapo ndipo ilipo. Kwa hivyo, kwa wanasayansi, kwa elimu, kwa kila kitu kilichopo ulimwenguni, ninaweka imani yangu juu ya Neno la Mungu na Hilo pekee.

30 Nimetoka katika malezi ya Kikatoliki, nikiwa Mwairishi. Watu wangu walionitangulia, sio baba na mama, bali kizazi cha pili, walitoka Dublin, Ayalandi, nao walikuwa—nao walikuwa Wakatoliki. Nilipokuwa...Nilimjua Mungu nilipokuwa mvulana mdogo, nilitaka kujua Mungu alikuwa Nani, nao watu wangu hawakwenda kanisani. Basi nikamwuliza kasisi habari za Mungu, naye akasema, “Mungu yuko katika kanisa Lake, hapo ndipo Mungu anapokaa. Huna budi kuwa mfuasi wa kanisa Lake.”

Nikasema, “Inanipasa kuwa mfuasi jinsi gani?” Bila shaka, ninyi Wakatoliki mnaelewa nilichoambiwa.

31 Ndipo nikaja kugundua kwamba...Nilicheza katika ujirani wa Wajerumani ambapo nililelewa, wa watu wanaoitwa Halman, Roderick, Fisher, Roder, na kadhalika. Nilikuwa ndiye wa pekee...Mimi na mvulana mmoja tulikuwa ndio wavulana Waairishi pekee katika shule nzima. Vema, hawa wavulana

wote walikuwa Walutheri, vema wakasema wao...kanisa lao lilikuwa ndilo kanisa. Ndipo nikaja kugundua kulikuwa na kanisa lingine lililoitwa Baptisti, Presbiteri, Anglikana. Loo, jamani! Vema, ni lipi kati ya makanisa hayo alilo ndani yake? Hilo ndilo nililojiuliza. Yuko wapi? Kama *hili* ni sahihi, *hili* halina budi kuwa limekosea, maana yanapingana. Sasa, ni lipi kati ya makanisa hayo ambalo Mungu yuko ndani yake?

32 Nikaketi, nikaanza kuisoma Biblia, nikiangalia maumbile. Nikaja kugundua ya kwamba Biblia ilisema kwamba "Yeyote atakayeondoa chochote kutoka kwenye Biblia hii, au kuongeza chochote Kwake, huyo ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima." Basi nikaona ya kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu siku moja kwa Yesu Kristo na Neno Lake. Sasa, kwa hiyo, ninaamini Biblia. Ninaamini Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Neno Lake, bali maadamu atafanya yale tu aliyo nayo katika Neno, basi ninaridhika na hilo.

33 Sasa, baadhi yenu ninyi ndugu, kumbukeni katika Agano la Kale, walikuwa na njia ya kujua kama nabii alikuwa anasema kweli, au mwotaji alikuwa akiota vizuri, ndoto yake ilitoka kwa Mungu. Walimpeleka kwenye hekalu, ambamo kifuko cha kifuani cha Haruni kilikuwa kinaning'inia, nacho kiliitwa Urimu na Thumimu. Wengi wenu ninyi watu mnajua habari zake, mkisoma katika Biblia. Ndipo wakati nabii huyu alipoanza kutabiri, nazo nuru hizo za kimbinguni hazikuangazia tena jambo hilo, kama upinde wa mvua uliofunika hapo, ukifanya Urimu na Thumimu kutoka kwenye kifuko kile cha kifuani, haidhuru yalisikika halisi jinsi gani, hawakuyaamini. La, bwana. Ilibidi yajibiwe na Mungu.

34 Sasa, Agano la Kale liliondolewa na kutimizwa, sio kuondolewa, bali kutimizwa. Basi lilipotimizwa, tukachukua Agano Jipya. Sasa, ile Urimu na Thumimu ya kale ilikuwa huko nyuma kwenye ukuhani wa Walawi, chini ya kifua cha Haruni, lakini wakati huu tuna mbao zingine mbili za sheria, Agano Jipya na la Kale. Na hizo ndizo Urimu na Thumimu ya Mungu kwangu. Ikiwa Mungu hatajibu kupitia Neno Lake tunapoona jambo fulani, basi ninaachana tu nalo. Lakini mradi tu ni Neno, basi ninajua ya kwamba mbingu na nchi zitapita bali Neno Lake halitashindwa kamwe.

35 Kwa hiyo, ninaamini Biblia kuwa ni Kweli halisi ya Mungu, Nayo si ya kuongezewa, wala kuondolewa, bali kuishiwa tu, kuhubiriwa katika urahisi Wake, kuishiwa jinsi ilivyoandikwa, naye Mungu, kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Na kama *Hili* ndilo Neno Lake, Naye alitoa ahadi ambayo hawezi kuiunga mkono, basi Yeye si Mungu.

36 Nami nimeona umbali huu, enyi marafiki, nina miaka thelathini na mmoja nyuma ya jukwaa, mimbara, sijawahi kuona

chochote alichoahidi ila kile ambacho angekifanya. Hiyo ni kweli. Nimemwomba vitu ambavyo sikupata, lakini sijawahi kumwomba, kwa kweli, chochote isipokuwa kile alichonipa au kuniambia kwa nini hakuweza kunipa. Kuna mambo mengi nisiyoyajua, mimi nina kikomo, Yeye hana kikomo, kwa hiyo, Mungu mkuu asiye na kikomo, nami, mtu mwenye kikomo, kuna mambo mengi ambayo ninatamani ambayo hayangekuwa mazuri kwangu kuwa nayo, kwa hiyo ninamtumaini tu Yeye, kama Baba yangu, kunipa yaliyo mema.

37 Nasi tuko hapa, usiku wa leo, kuomba pamoja nanyi, na kuzungumza nanyi kuhusu Neno, mikutano hii mitatu ijayo, kesho usiku na Jumapili alasiri, nami ninatumaini kwamba mtanipa usikivu wenu wa dhati, wala sitakaa popote ila moja kwa moja katika kurasa za Kitabu. Nami sihubiri Fundisho nje mikutanoni, niko huku nje kuudumisha Ujumbe rahisi, kuwaombea watoto wote wa Mungu. Nayo maswali ya kidini ambayo mnaweza kuwa nayo niani mwenu, ningekushauri umwulize mchungaji wako na si mimi, kwa sababu kila mtu anaongoza kundi lake. Na ikiwa yeye ni...huyo mchungaji amekuongoza salama umbali huu, mtumaini kwa safari iliyobaki. Yeye...Kama alikulea upate kujazwa na Roho wa Mungu, na kuishi maisha ambayo ninatumaini kwamba unaishi, mbona, mtumaini kwa safari iliyobaki, yeye, ataweza kuyajibu maswali yako.

38 Sasa, tukiliamini Neno, tuna ujumbe mdogo tu rasmi ambao tunatanguliza kila uamsho nao, na huo ni somo la, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kama... Sasa, tunajua ya kwamba hiyo ni Biblia, Waebrania 13:8. Na sasa, nina kipande kingine cha Maandiko ninachotaka kusoma, halafu, kinachopatikana katika Yohana Mtakatifu 12:20, na kuzungumza kwa dakika chache tu juu ya Maandiko, na kuwaombea wagonjwa, kujaribu kuwaruhusu mtoke mapema, kwa sababu najua watu wa mjini wana kazi za mjini, na lazima wazingatie saa. Wala hatuko hapa katika mojawapo ya ile miamsho mikubwa, lakini natumai kwamba siku moja tunaweza kurudi, ili tuwe na juma moja au mawili ambayo tutaweza... Lakini ni mkutano mdogo tu wa utangulizi.

39 Hamtaweza, hakika, kufahamu, nina hakika, maana kamili ya mkutano tunaouzungumzia, na jinsi Roho Mtakatifu... Lakini ninawaomba, kama rafiki yangu na kama mwaminio Mkristo hapa, usiku wa leo, ya kwamba utachunguza kile tunachosema kwa Maandiko. Na kama si cha Kimaandiko, basi ni jukumu lako kuniambia, kunionyesha mahali kimekosea. Na kama ni cha Kimaandiko, basi unawajibika kuyatii Maandiko.

40 Sasa, kabla hatujasoma, hebu na tuzungumze na Mwandishi tunapoinamisha vichwa vyetu. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nashangaa katika...hapa katika moyo wangu mwenyewe, usiku wa leo, kama kuna haja ambazo...

ulizo nazo moyoni mwako, ambazo unataka Mungu atimize wakati wa mkutano huu. Je, mwaweza tu kuinua mikono yenu, huku vichwa vyenu vimeinamishwa? Na moyoni mwako useme, "Bwana Yesu, nataka ujibu ombi langu katika mkutano huu. Nina mtu mgonjwa. Mimi mwenyewe ni mgonjwa. Nina rafiki aliyepotea, kaka, dada, mtoto, mume. Wakumbuke, Baba Mungu, wakati wa mkutano huu, jalia jambo fulani litendeke kwamba wataokolewa na kuponywa." Mungu awabariki.

41 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha neema wakati huu, na saa hii, tukiamini kwamba Utajibu kila haja. Tunakushukuru kwa ajili ya uaminifu huu, na kama. . .tunavyouita, kusanyiko "la kifalme" la Kanada. Pia Bwana, tunataka kuwa waaminifu kwa Mungu wetu. Kwa hiyo tumekusanyika huku nje katika alasiri hii yenye joto ili kumwabudu katika Roho wa Kweli Yake. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utabariki utu wetu.

42 Wabariki ndugu hao wanaouendeleza uamsho. Tunaomba ya kwamba utakuwa katika mikutano hiyo, Bwana, na uwape kwa wingi sana kupita yote wangeweza kufanya ama kuwaza.

43 Sasa, tunaomba, usiku wa leo, kwa ajili ya haja hizi. Watu hawa wana jambo fulani moyoni mwao, karibu kusanyiko lote usiku wa leo walikuwa wameinua mikono yao. Kuna kitu chini ya mkono huo, Bwana, moyoni. Hivi hutawajalia? Sasa, ninatoa maombi yangu, wanapoomba kimoyomoyo, ninakuomba kwamba. . .Ombi langu ni kwamba utajibu maombi yao. Ninaweka maombi yangu pamoja na yao juu ya Madhabahu Yako ya dhahabu pamoja na Sadaka hiyo, Bwana Yesu. Utusikie, Mungu. Alitwambia, "Mkimwomba Baba lolote kwa Jina Langu, nitalifanya." Sasa, tunaomba ya kwamba utatujalia haja hii, na utupe wakati mkuu, wa kupendeza, pamoja, tunaposhiriki kwenye Neno. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

44 Sasa, katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu 12 na ninii—ninii. . .tutaanzia kwenye kifungu cha 20, na kusoma kifungu cha 20 na cha 21.

> *Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:*
>
> *Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya,* wakamwomba *wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

Sasa, kwa ajili ya somo ningependa kuchukua hilo, *Sisi Tunataka Kumwona Yesu*. Andiko, Waebrania 13:8:

> *Yesu Kristo yeye yule jana,. . .leo na hata milele.*

45 Sasa, hebu na tuangalie moja kwa moja kwenye uso wa Neno la Mungu. Sasa, Biblia ilisema, hapa, ya kwamba

kulikuwa na Wayunani waliokwea kwenda kuabudu ambao walikuwa wamesikia habari za Yesu, nao wakaja, kwa mmoja wa wanafunzi Wake, waone kama wangeweza kumwona, nao wakapewa fursa hiyo. Sasa, ninii. . . Ni wangapi hapa wangependa kumwona Yesu, kweli tu kutoka moyoni mwako? Sisi sote. Mnaona mikono yangu? Vema, basi swali ni hili: Sasa, ikiwa Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na shauku yetu ni ile ile ya Wayunani, kwa nini hatuwezi kumwona? Mnaona? Na mnaona, huwezi kuifanya Biblia iseme jambo baya, kwa sababu haisemi. Sasa, kama Mungu ni Mungu, hana budi kusimama na Neno hili, hana budi kulitimiza Neno hilo kusudi awe Mungu.

46 Sasa, hawa Wayunani walitamani kumwona. Yeye hana upendeleo, Biblia inasema. Nao walitamani kumwona, nao wakapewa majaliwa ya kumwona. Sasa, Maandiko hayasemi walizungumza Naye, walimwona tu. Na hilo ndilo tunalotaka kufanya, tunataka kumwona.

47 Sasa, tunajua ya kwamba alikuwa. . . Aliteseka chini ya Pontio Pilato. Akasulubiwa, akafa, akazikwa, akafufuka siku ya tatu, kisha akapaa Mbinguni, na sasa ameketi mkono wa kuume wa ukuu wa Mungu Juu, anaishi daima kufanya maombezi tunapoungama; tunajua hilo. Na Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Tunajua Biblia inafundisha hivyo, Agano Jipya.

48 Sasa, kama shauku yetu usiku wa leo, kama kusanyiko la watu waliokusanyika pamoja. . . Kulikuwa na wawili tu wakati huo, nao wakaweza kumwona, na sasa, labda kuna mia moja na hamsini, nasi tunataka kumwona. Kwa hiyo kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hebu tumwone Yeye, na tuone kile alichokuwa.

49 Mnawazia Wayunani hao walikuwa wakimtafuta mtu wa aina gani? Je, walikuwa wakimtafuta rabi aliyevaa mavazi yake na kilemba? Vema, mtu yeyote angeweza kuvaa majoho na kilemba; mtu yeyote leo angeweza kufanya hivyo. Basi kama tulimwona mtu, na tulitaka kumwona Yesu, ambaye alikuwa Masihi, Kristo aliyetiwa mafuta, basi tungeweza kumwona mtu yeyote basi aliyevaa kilemba na ka—na kanzu kama vile wangewazia angevaa, kama kuhani, huyo angekuwa Yesu. Ingekuwa inachanganyisha sana basi, kuona watu wengi wanaovalia hivyo. Kwa hiyo hawakutaka kuona mavazi Yake.

50 Kwa hiyo labda, walitaka kuona kimo Chake, labda urefu Wake, jinsi angekuwa na mabega makubwa, au mtindo fulani a—alivyochanua nywele Zake, ama chochote kile; basi mtu yeyote angeweza kuiga hayo. Lakini walitaka kumwona Mtiwa-mafuta. Kwa hiyo ikiwa walitaka kumwona Mtiwa-mafuta, wange—wangekuwa wanamtafuta Kristo aliyetiwa mafuta.

51 Sasa, Biblia ilisema. . . Ninasoma katika Yohana Mtakatifu, tunarudi kwenye mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu tuone

kile hasa Yeye alichokuwa, tunakaribia kufikia katikati, mlango wa 12 sasa, wa Yohana Mtakatifu. Hebu turejee mwanzoni mwa Yohana Mtakatifu tuone kile Yeye alikuwa, na kama tunaweza kujua kile Yeye *alichokuwa*, basi tunajua Yeye *ni* nini. Je, hiyo ni kweli? Ndipo tutajua tunachotarajia.

52 Sasa, kama angekuja kwenye mji huu wa kupendeza, kwenye kisiwa hiki kinachovutia hapa, cha Victoria hapa, nasi tungekuwa tukimtafuta, nasi tunamtafuta usiku wa leo, na hii hapa ahadi Yake ya kwamba Yeye ni yule yule, basi hatuna budi kutafuta kujua kile tunachotafuta. Kama tungeninii, sisi . . . Ikiwa ni mavazi, labda tungeshuka twende tuone, labda, pengine kuhani wa kiorthodoksi huenda alivaa kama Yeye alivyovalia, ama—ama Myahudi fulani. Hakuvalia tofauti na mtu yeyote wa kawaida wa mitaani, lakini alivaa tu vazi la kawaida, hakuvaa nguo zozote za kidini, kwa sababu Yeye alitembea miongoni mwa watu, wala hawakutambua Yeye alikuwa ni Nani, kwa sababu alikuwa amevalia kama tu mtu wa kawaida. Ninaamini kama angekuwa hapa leo angekuwa Mtu nadhifu, avae suti, tai, kama tu mtu mwingine yeyote. Asingekuwa amejipamba mavazi ya kidini, siamini angefanya hivyo. Si—sidhani kama manyoya ndiyo yanayomfanya ndege, na ni asili ya ndege, maana ndege maridadi kuliko wote tulio nao ni wala mizoga. Kwa hiyo sisi . . . Manyoya hayafanyi ndege. Kwa hiyo ilikuwa ni kitu *Fulani ndani* Yake ambacho hawa Wayunani walitaka kuona. Na hicho ndicho tunachotaka kuona usiku wa leo. Tunataka kuona, si . . .

53 Sasa, kama tungesema, "Hebu tushuke mjini tuangalie kote, wananiambia Yesu yuko mjini, hebu twendeni tukamtafute." Kama tungeangalia, na kushuka mtaani, na kukuta mtu aliye na makovu mkononi mwake, na alama za misumari, na kwenye paji la uso wake, hapa, alikuwa na alama za miiba, na damu ilikuwa imetiririka usoni mwake, nasi tumwone na makovu ya misumari miguuni mwake, mnafiki yeyote angeweza kuwa nayo. Hakika. Mtu yeyote. Hatuna budi kutafuta kile alichokuwa, Utu wa Yesu. Kwa hiyo sasa, hebu tuone Kile Utu Wake ulichokuwa.

54 Sasa, Yohana alisema katika mlango wa kwanza, "Hapo mwanzo alikuwako Neno . . . " Sasa, neno ni wazo lililotamkwa. Ni wazo kwanza, unaliwazia, kisha unalitamka. Naye alikuwa Neno, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Je, hiyo ni kweli? "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno . . . " Hakika lilikuwa ni wazo Lake kabla hajalitamka, Nalo lilikuwa ni Mungu. Basi alipolitamka, likawa Mungu, kwa sababu Neno ni sehemu ya Mungu, kama vile tu wewe ulivyo sehemu ya neno lako. Basi alipolitamka, likawa Mungu. Naye huyo "Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu. Nasi tukamwona, Mwana pekee wa Baba, amejaa neema."

55 Sasa, kama Yeye alikuwa Neno basi, Neno lililotamkwa na

kudhihirishwa, basi ingebidi awe ni Kitu kile kile usiku wa leo, kwa sababu Mungu anaponena, hawezi kamwe kulighairi. Mnaona, hivyo ndivyo inavyokubidi kuwa na imani katika Biblia yako. Ni . . . Biblia yako ni hii: Mungu aliandika kwenye karatasi kwa mfano wa Neno, kwa sababu ni Mungu. Hata Agano la Kale, Biblia ilisema kwamba Neno la Mungu liliwajia manabii. Manabii, Neno la Mungu liliwajia.

56 Sasa, Yesu alipokuwa hapa duniani, aliwaambia wale ambao hawakumwamini . . . "Alikuwa mtu wa kawaida, naye alijiita mwenyewe Mungu." Akasema, "Unapojifanya sawa na Mungu tunajua wewe ni mwendawazimu." Nalo neno *wazimu* hapo, bila shaka tunaelewa, maana yake ni "kichaa." Na, "Una kichaa. Wewe ni Msamaria, una pepo," na kadhalika, lakini Yesu alisema, "Yachunguzeni Maandiko; kwa maana ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi." *Shuhudia* ni "kutoa ushahidi."

57 Unapoenda kwenye kesi kuwa shahidi, unatoa ushahidi kwa ajili ya mtu fulani. Unaona? Naye Yesu alisema, "Maandiko ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Basi Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa katika mwili wa mwanadamu. Mnaliona? Ahadi ya Mungu iliyofanyika mwili ili kujieleza Yenyewe, hivyo ndivyo Kristo alivyokuwa, Neno la Mungu lililodhihirishwa katika mfano wa mwanadamu. "Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu." Tena akawaambia, "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Lakini ingawa hamniamini Mimi, ziaminini hizo kazi." Mnaona, huyo ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa mwili. Yeye alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili, Neno, Neno lililo hai.

58 Hiyo ndiyo sababu, Wakristo, nafikiri ni halisi sana usiku wa leo, na ili kwamba tupate kuishi maisha yanayofaa, kwa sababu, mnaona, kunao watu wengi, hawatachukua nafasi kuisoma Biblia, bali watakusoma wewe. Unaona, wewe ni waraka ulioandikwa wa Mungu. Mkristo halisi, wa kweli, aliyezaliwa mara ya pili ni Neno lililodhihirishwa tena, kwa sababu ninyi ni nyaraka za Mungu zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote. Tunapaswa kuwa mtu wa aina gani, kama tunajua kwamba maisha yetu ni Biblia hai, iliyo wazi kwa asiyeamini, kumdhihirisha Mungu katika maisha yetu wenyewe? Angalieni. Sasa, tunaona "Yeye alikuwa Neno. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Sasa, tunaona ya kwamba, katika Waebrania, ninyi mnaoandika, Waebrania 4:12, Biblia ilisema kwamba, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, lachoma hata kugawanya, na mafuta ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo yaliyo moyoni." Neno la Mungu hutambua wazo lililo moyoni mwako. Kwa hiyo, Mungu usiku wa leo, akiwa ni Neno, anajua hasa hata unachowazia dakika ii hii. Kwa hiyo hivi mawazo yetu si yanapaswa kuwa safi, yaliyotakaswa, matakatifu, sikuzote

tukiwazia yaliyo bora zaidi?

59 Yesu akawaambia Mafarisayo, kasema, "Mnawezaje kunena mema? Kwa maana kutoka . . . " kasema, "enyi wanafiki," kasema, "kinywa hunena yaujazayo moyo." Mnaona, walikuwa wakiwaza jambo fulani mioyoni mwao na kusema jambo tofauti kwa kinywa chao, kwa hiyo hilo likawafanya wanafiki. Kasema, "Mnawezaje kunena mema, wakati yaujazayo moyo . . . " Alijua yaliyokuwa moyoni mwao. Mnaona? "Mwawezaje kunena mema, wakati mnapaswa kunena kutoka moyoni mwenu?" Kwa hiyo, hatupaswi kamwe kunena lolote isipokuwa lile tunaloamini na kuelewa, na liwe safi, na lisiloghoshiwa, na—na takatifu. Na mazungumzo yetu yawe mazuri na safi, mawazo yetu, tukiwazia yaliyo bora zaidi, tukiwaza mawazo ya Mungu, tukikaa juu ya mpango wa Mungu, na mbali na mambo ya ulimwengu.

60 Ni vibaya sana kwamba mambo ya ulimwengu yameliteka kanisa katika siku hizi. Naye Shetani alikuwa na njia mbovu ya kufanya jambo hilo, kuingiza televisheni moja kwa moja nyumbani, na kadhalika, na kuzipotosha akili za watu, na hata wa leo ambapo—ambapo asilimia kubwa ya kanisa, wanaojiita Wakristo, watakaa nyumbani wasihudhurie mkutano wa maombi, Jumatano usiku, waweze kuangalia kipindi fulani wakipendacho cha mtu fulani kutoka Hollywood, ama mahali fulani, ambacho hata hakipaswi kuwekwa kwenye skrini, labda akiishi na waume watatu au wanne, au wake, na kufanya yasiyofaa, na kuishi maisha ya kila namna, wanatoka wanaenda kwenye karamu za ulevi, na kuvuta sigara, na kusema uwongo, na kila kitu kibaya kinachoweza kufanywa.

61 Nayo makanisa yetu yanajirembesha yenyewe . . . hata mavazi yetu siku hizi yanafanana na Hollywood. Inasikitisha jinsi gani, kwamba nia zetu zinawazia . . . haziwezi kudumu safi na takatifu pamoja na Kristo. Imefanya jambo fulani kwa kanisa, imelilemaza, nalo limefanya jambo la kuchukiza sana, magazeti yetu yote, na kila kitu, yanaonekana tu kuwa yamepotoka. Lakini sikilizeni, enyi marafiki, ni katika saa hiyo ya upotovu, na wakati huo wa upotovu ambao Mungu anajitwalia Mwenyewe Bibi-arusi anayetoka katika upotovu huo. Hicho ndicho anachotafuta, kujipatia Kanisa linaloitwa kwa Jina Lake, Mtu anayetafuta Uzima usio na mwisho.

62 Vipi kama wakikupa, usiku wa leo, wakati ambao ungeweza kuishi miaka elfu kumi, na uwe ninii yote . . . mfalme juu ya dunia yote. Useme, "Je, ungeweza kubadilisha hilo na ujuzi wako, Bw. Branham?" La, bwana! Kama nikiishi miaka milioni kumi, wala nisiwe na siku moja zaidi ya umri wa miaka ishirini, na kuimiliki dunia nzima na vitu vyote vilivyomo, na kuhakikishiwa kutokuwa mgonjwa kamwe katika miaka milioni kumi, bado ningeirudisha mikononi mwao. Nina Kitu kikubwa zaidi ya hicho, nina Uzima wa Milele. Naam. Wakati hiyo miaka milioni kumi imekwenda kwenye Uzima wangu wa Milele,

mbona, hata haitakuwa kama. . . Kamwe haukuwa na mwanzo, kwa hiyo hauwezi kwisha. Ninakuwa mwana, nawe unakuwa mwana na binti wa Mungu, naye Mungu kamwe hakuwa na mwanzo, kwa hiyo Yeye hana mwisho. Kwa hiyo Neno la Mungu halina budi kudhihirishwa katika nafsi zetu wenyewe.

63 Sasa, sasa, tunaona ya kwamba Yesu alipokuja duniani. . . Sasa, ili kulidhihirisha Neno la Mungu, ilimbidi awe na—na—nabii, kwa sababu, daima, Neno la Bwana liliwajia manabii. Sasa, tunajua hilo. Sasa, Kumbukumbu la Torati mlango wa 18, nalo lilisema ya kwamba, Musa alisema, yule kiongozi mkuu ambaye wao. . . Mungu alikuwa amemchagua, na akamtuma chini akiwa na Nuru juu yake, Nguzo ya Moto, naye alikuwa amewaongoza wale watoto kuingia katika nchi ya ahadi, kulingana na yale aliyomwambia Ibrahimu miaka mingi hapo kabla, kisha akawaongoza kule, akasema, wakati wake wa kwenda, "Sasa, Bwana Mungu wenu atawaondokeshea kutoka miongoni mwa ndugu zenu, nabii kama mimi." Naye akaendelea na kuwaambia kwamba watu ambao hawatamwamini Nabii huyu watakatiliwa mbali na kusanyiko, nao wakamkataa, na hawakumwamini, nao wamekatiliwa mbali na kusanyiko. Hiyo ni kweli kabisa. Angalieni. Kwa hiyo hapana shaka Yeye ni nabii.

64 Na kama ukisoma katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema Mwenyewe, baada ya kupita kando ya birika la Bethesda, na huko akamkuta mtu huyu amelala hapo, nao wakamhoji juu ya kuwaponya hao wengine, ama chochote walichofanya, akasema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile *amwonalo* Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile." Sasa, je, mnaamini ya kwamba hayo ni Maandiko yaliyovuviwa ya Mungu? Basi Yesu kamwe hakufanya mwujiza hata mmoja, wala kufanya lolote, mpaka kwanza kwa ono akamwona Baba akilitenda. Huwezi kumfanya aseme uongo, na kumwacha abaki kuwa Mungu. Unaona?

65 Kwa hiyo huna budi kuliamini Neno, jinsi tu lilivyoandikwa. Hakuna kujipinga ndani Yake. Nimeuliza kote katika miaka mtu mmoja anionyeshe ukinzani, haupo, ingawa Kitabu kizima cha sitini na sita, kilichoandikwa na manabii mbalimbali walioachana kwa mamia na mamia ya miaka na kadhalika, bali kila Neno huja moja kwa moja na linaumana tu namna *hiyo*. Hiyo ni kweli. Hayajipingi, halifanyi hivyo. Kwa hiyo tunaona kwamba Neno ni kweli. Hivyo ndivyo unavyoweza kuwa na imani, si katika kanisa, katika madhehebu fulani, bali katika Neno, Hicho ndicho Kitu ambacho hakitapita.

66 Na kama Mungu akiwahi kuitwa jukwaani kufanya uamuzi, na uamuzi anaofanya mara ya kwanza hana budi kubaki na uamuzi uo huo. Sasa angalieni, mimi na wewe tunaweza kufanya uamuzi, na labda baada ya kitambo kidogo tuone kwamba tulikosea, kwa hiyo tunafanya uamuzi mwingine, ni bora

zaidi. Baadaye tunagundua tulikosea hapo, tunafanya uamuzi mwingine, kwa sababu sisi ni wenye kikomo, wanadamu wa duniani, viumbe vya wakati. Lakini Mungu hana kikomo, hivyo hawezi kufanya uamuzi bora zaidi, kwa sababu kila uamuzi ni mkamilifu. Kama ni. . .Na kama Yeye. . .Ikiwa sivyo. . . Kama aliitwa jukwaani kumwokoa mtu, na juu ya msingi aliomwokolea mtu huyo, hana budi kudumu milele na msingi uo huo ambao alimwokolea mtu wa kwanza. Asipofanya hivyo, basi Yeye alifanya makosa wakati alipotenda mara ya kwanza, ndipo basi ingebidi useme Mungu alikosea.

67 Sasa, ungeweza kusema, "Nimekosea, sikupaswa kufanya hivyo. Nitalifanya kwa njia yako, nilifanye kwa njia hii nyingine." Sasa, huyo asingekuwa ni Mungu? Mungu hana kikomo. Je, ni msingi gani ambao Mungu alimwokolea mwanadamu kwa mara ya kwanza? Chini ya damu iliyomwagika, wala hajawahi kuubadilisha, na kamwe hataubadilisha. Naam, bwana. Damu ndiyo iokoayo.

68 Bustani ya Edeni, kulikuwa na mnyama asiye na hatia aliyeuawa, akamwaga damu kuwaokoa. . .Adamu na Hawa kutoka kwenye mateso huko ng'ambo, kuzimu. Damu isiyo na hatia! Na leo, ingawa tumejaribu kuwaelimisha watu kwake, tumejaribu kuwateulia watu kwake, tumejaribu kufanya kila kitu, nasi tunaona kwamba tunawatenganisha watu. Lakini chini ya Kitu kimoja, Damu iliyomwagika, sote tunaweza kuwa ndugu na dada katika Kristo. Bado ni Damu iliyomwagika ya Yule asiye na hatia ndiyo inayookoa.

69 Uponyaji wa Kiungu uliwekewa msingi juu ya. . .Mara ya kwanza Mungu alipopata kuitwa jukwaani kumponya mtu, jambo la kwanza, tunaelewa, lilikuwa ni ulaji wake, na alipofanya hivyo aliuweka juu ya msingi wa, "Ikiwa utaamini. . ." na hajawahi kuubadilisha tangu wakati huo. Ni imani katika ahadi ya Mungu, na kwa hiyo, lazima ibaki vile vile. Ni. . .

70 Mnaona, katika dhabihu ya Ibrahimu, Yeye alitenganisha, wakati alipofanya thibitisho, katika mlango wa 16 wa Mwanzo, wakati alipowachukua wale, mbuzi jike na ndama na kuwapasua, kwa sababu vipindi vya wakati vilitoka kwenye mwana-kondoo wa kawaida ikawa ni Mwana-kondoo wa Mungu. Lakini je, mliona, njiwa na hua Yeye kamwe hakuwapasua? Na daima iliwakilisha uponyaji wa Kiungu, kwa maana wakati mwenye ukoma ama kitu fulani aliposafishwa, walimwua ndege mmoja, na kumwaga damu juu ya huyo mwingine, na mabawa yake, akatoka nje akilia, "Mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana," akiinyunyizia ardhi kwa ajili ya upatanisho. Nao ndege hawakutenganishwa, kwa sababu walijumuishwa katika upatanisho. Na kama upatanisho wa kale ulikuwa na uponyaji wa Kiungu ndani yake, ni zaidi sana

vipi Upatanisho huu ulivyo mkuu zaidi, Ule mpya? Mnaona? Kwa hiyo hakuna swali juu yake kwa Mungu.

71 Sasa, Huyu hapa, alikuja kulitimiza Neno la Mungu. Ili kulitimiza Neno la Mungu, ilibidi awe Dhihirisho la Neno la Mungu. Sasa, angalieni tunachopata. Tukirudi nyuma, tungeweza kuchukua muda mwingi, lakini hatutafanya hivyo, tutaokoa wakati, tukiweza. Angalieni. Tunaona huduma Yake ikianzia hapa, katika Yohana Mtakatifu, nasi tunaona. . . Tunajua kuzaliwa Kwake, na jinsi alivyotoka nyikani, akabatizwa na Yohana, kisha akaenda nyikani, naye akajaribiwa na ibilisi muda wa siku arobaini, kisha akatoka nyikani, na mara ishara kuu na maajabu yakaanza kuingia.

72 Sasa, Yohana alishuhudia, aliona ishara ya Masihi. Sasa, Yohana hakwenda shuleni kujifunza jambo hili, ingawa baba yake alikuwa kuhani. Baba yake alikufa alipokuwa na umri wa karibu miaka tisa. Badala ya kufuata mkondo wa kawaida wa baba yake kuwa kuhani, na kadhalika, na shule zote, kazi yake ilikuwa muhimu sana, hana budi kuwa mtangulizi wa Masihi; alikuwa awe ndiye atakayemtambulisha. Alitabiriwa, na nabii Isaya, miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, "Kutakuwa na sauti ya mtu nyikani, akilia." Na pia miaka mia nne kabla ya kuzaliwa kwake, Mika, yule nabii wa mwisho, alisema, "Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, akaitangaze njia." Kwa hivyo lazima asichukue wazo la shule yoyote juu yake, hana budi kwenda nyikani. Ndipo alipotoka akarudi, alikaa hapo mpaka akawa na hakika kwamba aliijua ile ishara, na haya ndiyo aliyosema: "Yeye aliyeniambia, kule nyikani, niende nikabatize kwa maji, alisema, 'Yule ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.'" Ilimbidi kuwa na hakika.

73 Basi enyi marafiki, kama Kristo alikuwa anakuja, naye Yohana ilimbidi kuwa na hakika na kile alichokuwa akifanya, hebu hili lizame ndani kabisa ya moyo wako, hatuna budi kuwa na hakika na *hili*. Kuna mambo ya kila namna yanayoendelea, lakini lazima tuwe na hakika. Hupati nafasi kurudi na kujaribu tena, lifanye sasa la sivyo hutawahi, huu ndio wakati wako.

74 Sasa, Yesu mara moja. . . Kulikuwa na mtu jina lake Andrea, mtu mashuhuri, mtu mzuri, mvuvi; yeye na ndugu yake, Simoni, walivua samaki pamoja. Kwa hiyo wakasikia habari za huduma ya Yohana, na kwa hiyo, kwa kuwa walikuwa watu wa dini, walikuwa wameyasoma Maandiko, pamoja sana, na kujua ya kwamba alikuwa yuaja Masihi.

75 Baba yao, Yona, alikuwa M—Mfarisayo, mwalimu. Nami. . . Kama tunavyoambiwa, siku moja aliketi kando ya meli yake ndogo, akawaambia Andrea na Petro, "Wavulana wangu, sikuzote niliwazia kwamba ningeishi kumwona Masihi." Lakini

huku mvi zake zikipeperushwa na upepo, na ngozi yake iliyojaa makunyanzi, akasema, “Nitakusanywa pamoja na watu wangu, kwa hiyo nadhani sitamwona, lakini labda mtamwona katika siku zenu. Sasa, wanangu, ajapo Masihi, kabla tu ya Kuja Kwake kutakuwa na kila kitu kikitukia, kila namna ya ‘Masihi.’ Lakini msidanganyike, wanangu, kumbukeni, Biblia inatufundisha, Musa, nabii we—wetu, anatufundisha kwamba ajapo Masihi, atakuwa nabii, si mwelimishaji, si mwanachuoni, nabii, Mfalme-Nabii, ambapo karama hizo zote kuu zilizokuwa ndani ya manabii hao wote zitakusanyika katika—katika Uungu mmoja. Mnaona? Atakuwa Mfalme-Nabii. Nanyi hamna budi kukumbuka, kwamba Musa alitwambia tusidanganyike, bali Bwana Mungu angemwinua huyu Masihi, naye angekuwa nabii.”

76 Basi Yohana alipokuja, walimwuliza, akasema, “Wewe ndiye *yule* Nabii?”

77 Akasema, “Mimi siye. Lakini Yeye anakuja nyuma yangu, sistahili kubeba komeo la viatu Vyake. Anakuja nyuma yangu, mimi siye Nabii *yule*, lakini atakuja nyuma yangu. Nami nawaambia ya kwamba Yeye yuko miongoni mwenu sasa, wala hamjui.” Naye alikuwako. Kasema, “Kuna Mtu amesimama miongoni mwenu sasa hivi msiyemjua, Yeye Ndiye.” Alikuwa na hakika sana kwamba alikuwa akiishi katika siku hiyo kabla tu ya . . . Alijua kazi yake ilikuwa ni kumtangaza Masihi. Basi alipokuwa akitangaza Kuja kwa Masihi, alijua ilibidi iwe katika wakati huo, papo hapo. Hivyo akasema, “Yeye yuko miongoni mwenu, Yuko duniani leo. Amesimama miongoni mwenu.”

78 Jamani, ilikuwa ni nini sasa . . . Hilo si lingeleta mtego kwa madhehebu yote ya siku hiyo? “Vema, hapa tuna Dk. *Nanii*, Rabi *Nanii*. Angalieni jinsi alivyo kijana wa kupendeza. Angalieni jinsi anavyochanua nywele zake, jinsi anavyozungumza kwa ufasaha. Mbona, yeye—mbona, alihitimu . . . Alipata Shahada yake ya Sanaa alipokuwa na umri wa miaka kumi na mitano tu. Vema, unajua huyo ndiye Masihi.” Mnaona?

79 Lakini Yohana angetikisa kichwa chake. Akasema, “Yeye aliyeniambia, huko nyikani, niende nikabatize kwa maji alisema, ‘Yule nitakayemwona Roho, akishuka, Nuru hii ikishuka kutoka Mbinguni, na kuja juu Yake, Huyo Ndiye. Nangojea kumwona.” Siku moja akatoka akaenda huko nje, Naye huyo hapo, akamwona. Mtu asiye na elimu, hakuwahi kwenda shule hata siku moja maishani Mwake, hatuna taarifa Yake ya kwenda shuleni, kamwe hakuandika Kitabu. Hamna kitu. Ni vigumu kwetu kujua . . . Yeye alijitokeza tu, akaondoka vivyo hivyo, lakini Yeye alikuwa Imanueli.

80 Hapa Andrea alikuwa akiifuatilia mikutano hii, kumsikiliza Yohana, naye akasimama pale siku hiyo na kumsikia Yohana akisema, “Tazameni Mwana-kondoo wa Mungu, aondoaye dhambi ya ulimwengu.” Yohana amesimama pale akishangaa,

akitazama Kitu fulani, Hii hapa ikishuka, Sauti, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye nimependezwa kukaa ndani Yake." Hakuna mtu mwingine aliyeisikia, hakuna mtu mwingine aliyeiona, ila Yohana alishuhudia ya kwamba aliiona. Kwa nini? Aliahidiwa. Walimwengu wengine wasingeweza kukaa hapa, usiku wa leo. Umeahidiwa kitu, nawe unakitarajia. Hiyo ndiyo sababu Yeye anajifunua Mwenyewe vivyo hivyo.

81 Kwa hiyo walikuwa wakitazama. Naye Yohana akashuhudia. Andrea akaenda nyumbani, akamwambia Simoni usiku huo, "Tumempata Masihi!"

82 Vema, naweza kuwazia Simoni akisema, "Sasa, ngoja kidogo, Andrea, tumefundishwa bora zaidi ya hilo. Sasa, Nabii fulani wa nyikani, *anavyojiita*, huko nje . . . Loo, lolote usemalo."

83 Basi siku moja, Simoni akaenda pamoja naye Mbele za Bwana Yesu. Sasa, Simoni hakuwa na elimu. Tunajua Biblia ilisema hakuwa na elimu wala maarifa; hakuweza hata kuandika jina lake mwenyewe. Hiyo ndiyo aina ya mtu ambaye Mungu alimchagua. Basi ikiwa elimu ni sehemu kubwa hivi, kwa nini Yeye . . . kwa nini alimchagua mtu kama huyo ili ampe funguo za Ufalme? Mnaona, tunaiacha njia. Sasa, siungi mkono kutojua kusoma na kuandika, ninataja tu ukweli wa mambo. Mungu anataka moyo mnyenyekevu. Ni afadhali watoto wangu wamjue Yesu Kristo kama Mwokozi wao, na hata wasijue jinsi ya kuandika jina lao, kuliko kuwa na . . . kuliko kuwa mwalimu bora aliyeko kote ulimwenguni. Hiyo ni kweli. Angalieni. Kwa maana huo ndio Uzima wa Milele, kumjua Yeye.

84 Huyu hapa. Simoni alikwenda Mbele Zake. Kasema, "Hebu njoni tu mkamsikilize wakati mmoja. Ataanza kuhubiri sasa katika siku chache, maana Yeye alitoka nyikani. Nao watu wameanza kuja, Yeye ameanza kuwaombea wagonjwa, nao wanapona. Basi Huyo si atakuwa ni Masihi?"

"Sasa, angalia hapa, Andrea, Masihi, kulingana na Neno, atakuwa nabii."

"Vema, ninaamini Yohana alikuwa nabii."

"Alionyesha ishara gani alikuwa ni nabii?" Aliongea tu. Mnaona? Vema.

85 "Lakini njoni kwa Mtu huyu." Sasa, huyu hapa anakuja Simoni Pet- . . . Simoni akaenda Mbele Zake. Ndipo mara Yesu alipomwona, alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hilo lilitosha. Alijua papo hapo Huyo alikuwa ndiye Masihi. Kwa nini? Sio tu kwamba alimjua, bali alimjua yule baba yake mzee mtauwa, ambaye alikuwa amemdumisha katika Neno. Mnaona jinsi yote yanavyoumana? Simoni Petro upesi akatambua ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi, kisha akapewa funguo za Ufalme.

86 Palikuwa na mtu mmoja amesimama hapo, jina lake Filipo. Alikuwa ni msomaji wa Biblia pia, naye pamoja na mtu aliyeitwa Andrea walikuwa na ushirika mwingi, kama ninyi watu, mkienda nyumbani . . . Ikiwa mnaamini . . . Ni wangapi wenu mnasoma pamoja, mnalisoma Neno? Nanyi mnaenda nyumbani, na kuchunguza Maandiko. Nao walihusika juu ya wakati ambao walikuwa wakiishi, kwa hiyo wakachunguza Maandiko kwa makini sana. Basi walipofanya hivyo, walipata kujua kile alichopaswa kuwa. Ndipo Filipo alipoona hilo, hilo lilitosha kwake. Huyo akazunguka mlima, ambapo ni kama maili kumi na tano kuuzunguka mlima. Ikiwa umewahi kuwa Palestina unaweza kuyaweka hayo maeneo alama. Ndipo akazunguka siku moja na kurudi kesho yake.

87 Sasa, alipompata Nathanaeli, alikuwa kwenye shamba la matunda huko nje, katika kijisitu chake cha mitini, naye alikuwa huko nje akiomba. Na, hivyo basi huyu hapa Filipo anakuja kumtafuta, akamkuta amepiga magoti akiomba, akimwomba Mungu, akiisha kumaliza kuomba, akasimama. Naye akasema, "Nathanaeli, njoo uone Yule tuliyempata. Tumempata Masihi aliyenenwa na Musa, Nabii ambaye Musa alisema Bwana Mungu wetu atamwinua. Tumempata!"

Ninaweza kuwazia Nathanaeli akisema, "Filipo, unataka kusema nini? Ati nani Huyo?"

"Ni Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu."

88 Sasa, hilo lilimzidia sana jamaa huyo. Akasema, "Je, laweza neno lolote jema kutoka Nazareti, kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha, au," samahani, "watu huko chini? Je, laweza neno jema kutoka kwao? Mbona, tunajua kama linatoka popote lingetoka kwenye dhehebu letu. Laweza neno lolote jema kutoka huko?"

89 Sasa, Filipo akampa jibu zuri zaidi ambalo mtu yeyote angeweza kumpa, akasema, "Njoo, uone." Usikae nyumbani na kukosoa, njoo, chukua Maandiko, upate kujua kama ni kweli au la.

90 Naweza kusikia maongezi yao wakienda zao njiani. Naweza kumsikia Filipo akisema, hapa, kwa—kwa Nathanaeli, kasema, "Nathanaeli, unakumbuka wakati ule uliponunua samaki, kule chini mtoni, kutoka kwa yule mvuvi mzee, jina lake Simoni, ambaye asingeweza kukutilia sahihi ile risiti?"

"Naam, namkumbuka."

"Vema. Sasa . . ."

"Loo, nilimjua baba yake, nilinunua samaki kutoka kwa Yona, baba yake. Ana mtoto wa kiume jina lake Andrea."

91 "Naam, wote wawili ni waaminio. Basi mara Simoni alipokuja Mbele za Masihi huyu, alimtazama usoni, akamwita Simoni, na kumwambia jina la baba yake. Sasa, tunajua

Maandiko yanasema ya kwamba Bwana atamwinua Nabii. Nasi ni Wayahudi, na tunajulikana kuwaamini manabii wetu. Nayo Biblia yetu inatwambia hapa pia ya kwamba akiwepo mtu wa kiroho au nabii miongoni mwenu, Mimi, Bwana, nitanena na nabii huyu, na asemayo yakitimia, basi msikieni, na yasipotimia, basi msimsikie. Basi huyu hapa Mtu ambaye asemacho kinatokea papo hapo kikamilifu kuthibitisha kwamba ndivyo ilivyo. Isingenishangaza kama hakukuita, ulipofika mbele Zake."

92 Vema. Walipofika Mbele Zake, Yesu labda alikuwa akiendesha mstari wa maombi, ama chochote kile, huenda alikuwa amesimama huko nje kwenye kusanyiko, lakini popote ilipokuwa, Yesu alipomkazia macho yake, alisema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!" Hilo lilimpunguzia majivuno.

Akasema, "Rabi, ulinijuaje?" Sasa, wote walivaa kwa namna moja, walikuwa na ndevu na vilemba na majoho. "Rabi, ulinijua lini?"

Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Loo, macho ya jinsi gani! "Nilikuona chini ya mtini."

93 Mwajua nini, huyo mtu aliyefunzwa wa Maandiko, Uzao huo uliochaguliwa Uzima wa Milele tangu zamani, Nuru hiyo ilipomwangazia, alisema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli." Sio mavazi Yake yaliyofanya hivyo, si kimo Chake kilichofanya hivyo, mtindo wa nywele Zake, jinsi alivyochana ndevu Zake, bali Roho aliyekuwa ndani Yake alionyesha ya kwamba ni Mungu, Neno, lililofanyika mwili, kwa sababu lingeweza kuyatambua mawazo yaliyo moyoni. Huyo alikuwa ni Yesu jana. Na kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, atakuwa yeye yule. Hivyo ndivyo angekuwa siku hizi. Hiyo ni kweli? Kama huyo alikuwa ni Yesu, ingekuwa ni Kristo yeye yule.

94 Mnaona, kama nilivyosema siku kadhaa zilizopita usiku, kama ungeweza kuondoa uhai wote kutoka kwenye mpichi, na kuhamisha uhai wa mpea ndani ya mpichi, ungezaa mapichi. Hakika. Aina ya uhai uliomo ndani yake, huo ndio unaozaa. "Kwa matunda yao mnawatambua." Yesu alisema katika Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya . . ." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

" . . . Mwana wa Adamu, Malaika wakipanda na kushuka," na kadhalika.

95 Uko katika—uko mahali panapostahili. Umejiweka mahali pako, kwa kumtambua Yeye, kwamba uko—uko tayari sasa kuona mambo makubwa zaidi. Loo, kama tungeweza kujiweka katika nafasi hiyo ya kumtambua, basi tutaona uponyaji ukifanyika mwilini mwetu, ndipo tutaona furaha ikiingia, na tutaona mambo makubwa yakitokea.

96 Sasa, labda huenda ikawa kuhani wake alikuwa amesimama pale. Loo, kulikuwa na wale waliosimama pale ambao hawakuamini, walimu wa siku hizo, wamesimama pale huku wameweka mikono yao nyuma yake. Walijua iliwabidi kulijibu kusanyiko lao. Lilikuwa tayari limefanyika. Mnajua walichosema? Walisema, "Jamaa huyu ni Beelzebuli, ibilisi, mpiga ramli."

97 Naye Yesu akasema, "Nimewasamehe kwa kuniita Mimi ninii . . . hivyo, lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya jambo lile lile, na kusema neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Hivyo ndivyo dhambi- . . . ndivyo ilivyo katika siku hii ya mwisho. Tumekuwa na miaka elfu mbili ya mafundisho. Huyo hapo. Jinsi tungeweza kuendelea na wahusika hawa, lakini kwa sababu ya muda, labda tutalichukua kesho usiku tena.

98 Angalieni. Hiyo ndiyo njia. Sasa, kumbukeni, kulikuwa na wale pale waliokuwa ni watu watakatifu, walikuwa watu wazuri, walikuwa walimu. Lakini Yesu akasema, "Mnazunguka bahari kupata mwongofu mmoja, ndipo mkimleta zizini mwenu, yeye ni mtoto wa kuzimu mara mbili kuliko alivyokuwa hapo mwanzo," akasema, "kwa sababu mnazibatilisha amri za Mungu kwa mapokeo yenu."

99 Na hiyo ndiyo shida yake siku hizi, tumechukua mapokeo yao na kuyaongeza kwa kanisa, badala ya kuchukua yale ambayo Mungu alisema. Mnaona? Sasa, mnajua ya kwamba Yesu Kristo hakuja kwa njia mbaya, Yeye alikuja sawasawa kabisa, jinsi Biblia ilivyosema angekuja. Lakini mapokeo yao yalimweka katika madoido mengine ya Kristo, Naye alikuja akiwa maskini na mnyenyekevu, vile vile hasa Biblia ilivyosema angefanya. Naye alifanya jambo lile lile hasa, na akaonyesha ishara Yake ya Kimasihi jinsi hasa Biblia ilisema. Lakini hawakufundishwa kuliamini hivyo. Mungu, usituruhusu kuliruka wakati huu. Jalia tuwe na mioyo iliyo wazi na akili iliyo wazi kusikiliza.

100 Lifanye Neno . . . Yeye alikuwa Neno, naye Neno alikuwa Mungu, naye Neno alifanyika mwili. Nalo Neno lile lile liliahidi, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi," na *mimi* ni kiwakilishi nafsi, "Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Kweli. "Na kazi nizifanyazo, mtafanya jambo lile lile. Msitafakari mtakachosema, kwa sababu si ninyi mnenao, ni Baba, Roho Mtakatifu aishiye ndani yenu, Ndiye anenaye. Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe." Yeye aliona ono.

101 Sasa, jambo lile lile linatumika tena siku hizi. Yote aliyokuwa Mungu aliyamimina ndani ya Kristo, yote aliyokuwa Kristo aliyamimina ndani ya Kanisa. Ni Mungu yeye yule wakati wote. Mungu juu yetu, asingeweza kuja karibu nasi kwa sababu tulikuwa wenye dhambi. Damu ya wana-kondoo

isingeweza kuondoa dhambi, lakini basi, Mungu alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Tunaamini hilo. Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Mkristo yeyote anaamini hilo.

102 Siku hizi wanapojaribu kumfanya kuwa mwanafalsafa tu au mwalimu, linanichefua tu. Yeye alikuwa wa Kiungu, alikuwa zaidi ya mwalimu, ama—ama mwanafalsafa, alikuwa Imanueli. Mungu alijiumbia Mwenyewe mwili, Mwanawe, kisha akashuka na kukaa katika mwili huo, Mungu ndani ya Kristo. "Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu. Yeye hunionyesha la kufanya, nami ninatenda tu katika Uwepo Wake, mahali Pake." Yohana Mtakatifu . . . Loo, jamani! Ni rahisi tu, mnaona, kuona kile anachozungumzia.

103 Tazama. Alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Ninatoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu." Hiyo ni kweli? Sasa, mwalimu yeyote anajua ya kwamba ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wale wana nyikani, ama nyika-. . ., ama, wana wa Israeli waliifuata Nguzo hiyo ya Moto, ya kwamba Huyo alikuwa ni Kristo. Nyote mnaamini hilo, sivyo? Alikuwa Malaika wa Agano.

104 Musa aliiacha Misri, "Akihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni hazina kuu kuliko hazina ya Misri." Ilikuwa ni Kristo. Basi, huyu hapa Malaika yule, alikuwa katika . . . Vema, Yeye alisema jambo lile lile. Akawaambia, akasema hata . . . Alikuwa . . . "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." MIMI NIKO Ndiye aliyekuwa pamoja na Musa, nyikani, kwenye kile kichaka cha Moto, "Kabla," Yohana Mtakatifu 6, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Na hilo lilikuwa kumbukumbu kwa vizazi vyote. Sio, "Nitakuwa, nilikuwa," "MIMI NIKO," wakati uliopo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kifo Chake, kuzikwa, kufufuka . . .

105 Ndipo mtu mmoja, jina lake Sauli, alikuwa akienda zake Dameski kuwakamata watu waliokuwa katika njia hii. Na yapata adhuhuri alipigwa akabwagwa chini na Nuru, Nuru ile ile. Haiwezi kubadilika. Inambidi kubaki vile vile. "Ninatoka kwa Mungu," akafanyika mwili, "Ninaenda kwa Mungu." Amina.

Unajuaje kuwa alikuwa ni Mungu yeye yule? Alisema, "Bwana."

Alisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu."

106 Ilikuwa ni Yeye aliyekuja usiku ule, Nuru hiyo, na kufungua pingu za Petro, na kulifungua lango, na kumtoa nje, Malaika wa Bwana. "Ninatoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu," ikimfanya Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye yuko pamoja nasi usiku wa leo, Mungu yeye yule.

107 Angalieni, katika Ibrahimu, Yeye aliwaonyesha ishara wakati wote hata kwa Ibrahimu, lakini hatimaye akaja kwenye ile ishara kuu ya kumalizia.

108 Sasa. Sasa, kumbukeni, tumeketi hapa usiku wa leo. Ninaona baadhi, marafiki zangu Wahindi kutoka juu hapa, chini. Hao ni Wahindi, hawa hapa Wajerumani, Waswidi, Waairishi, watu wa kila namna, ama wale tunaowaita mataifa. Lakini kuna ninii tu...Sisi sote tumetoka kwa mtu mmoja, Adamu. Na kuna jamii tatu tu ulimwenguni kote, nazo ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Kwa maana kutoka kwa hao watatu...Baada ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika hapakuwa na mtu duniani.

109 Basi angalieni, Petro akiwa na zile funguo. Aliwafungulia Wayahudi kwenye Pentekoste, Wasamaria, na kisha kwa Kornelio. Ndipo basi tangu hapo na kuendelea, ilikuwa kwa kila mtu. Mnaona? Hao ni Wayahudi, Wasamaria, na Wamataifa. Sasa, angalieni, Wayahudi na Msamaria...Msamaria alikuwa nusu Myahudi na Mmataifa. Kwa hiyo walimwamini Mungu, bali walikuwa wakimtazamia Masihi. Na endapo wanamtazamia Masihi, basi Yeye anawajibika kuwajia. Amina. Ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi. Kujua kwamba Yeye hutimiza ahadi Yake.

110 Sasa, Yeye alikuja kwa Myahudi, Myahudi aliyechaguliwa, Naye akafanya ishara Yake ijulikane mbele yao wote. Baadhi yao walisema, "Huh, Beelzebuli. Yeye ni mpiga ramli," kuyaita matendo ya Mungu pepo mchafu, ambaye angeweza kutambua mawazo. Bila kujua ya kwamba Neno ni Mtambuzi wa mawazo, Nabii, Yule...Neno la Bwana lilimjia nabii, linamfanya kuwa Neno kwa sehemu. Kama tulivyo usiku wa leo, visehemu vya Neno. Yeye alikuwa na Neno kamilifu; Utimilifu wa Mungu ulikuwa ndani Yake. Alikuwa Naye bila kipimo; tunaye kwa kipimo, bali ni Roho yeye yule.

111 Angalieni. Naye Huyu hapa amesimama, akifanya hasa ile ishara ya Kimasihi, na mmoja tu mara kwa mara, wa Wayahudi, angemwamini. Sasa, kulikuwa na wale pale ambao wasingeweza kumwamini, wala usingeweza kusema hawakuwa watu wazuri. La, bwana. Walikuwa watu wazuri, iliwabidi kuishi maisha mema. Usingeweza kusema hawakuwa waaminifu na wanyoofu; wala wasingeweza kudanganya, wala kuiba. La, bwana. Lakini mambo hayo hayakuokoi, si kwa matendo mema tunaokolewa. Kama matendo mema yangefanya hivyo, isingalimlazimu Kristo kufa. Mnaona, ni kuzaliwa. Huna budi kuzaliwa mara ya pili, huna budi tu. Hakuna njia kabisa ya kulikwepa, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, kamwe hatauona Ufalme."

112 Sasa angalieni, dhambi si kusema uongo, kuiba, kunywa pombe, kufanya uzinzi, hiyo siyo dhambi, hayo ni matokeo ya kutokuamini. Dhambi pekee iliyopo, ni kutokuamini. Haki

pekee iliyopo ni, ni imani. Imani na kutokuamini, hivyo ndivyo vyanzo viwili inakotoka. Ye-. . .Biblia ilisema, "Asiyeamini amekwisha hukumiwa."

113 Hivyo basi, wapi. . .jinsi walivyo wa kidini. . .Budha: wa kidini, hao Waislamu ni waaminifu kadiri siku zilivyo ndefu. Mnaona? Hakika. Wao ni wa kidini, watu wema, wazuri, ila ni wasioamini, kwa hiyo hilo linawafanya kuwa mwenye dhambi. Na mtu yeyote asiyeamini kila Neno la Biblia hii, roho iliyo ndani yako ni mbaya. Roho Mtakatifu aliiandika Biblia, alisema hivyo. Waebrania mlango wa kwanza ilisema, "Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliiandika Biblia." Kweli. Kwa hiyo Roho Mtakatifu aliiandika Biblia. Je, Yeye anaweza kugeuka, na kuikana, ama kuingiza kitu ndani Yake ambacho hakikuwa sahihi? Roho Mtakatifu halisi katika maisha ya kila mtu ataitikia kila kifungu katika Biblia hiyo kwa "Amina." Roho Mtakatifu halisi, anaiamini.

114 Sasa, Wasamaria hawa walikuwa wakimtazamia Masihi. Wayahudi walikuja, Yeye akajionyesha Mwenyewe kama Masihi. Ndipo alipofanya jambo hilo, walitambua kuwa Huyo alikuwa ni Masihi. Wengine hawakutaka, kwa sababu kanisa lao liliwazuia wasifanye hivyo. Vema, mnajua kilichotokea. Halafu kulikuwako na Wasamaria fulani. Siku moja, Yeye alikuwa hapa juu Yerusalemu naye alikuwa akishuka kwenda Yeriko, ambao ulikuwa moja kwa moja chini ya mlima, moja kwa moja njiani kuelekea Yeriko, lakini alihitaji kupitia Samaria. Hiyo ingekuwa ni kama mimi kwenda nyumbani kwangu huko Indiana kwa kupitia njia ya California, kwenda mbali na njia yako. Ninaishi upande *huu*, California, nadhani, iko upande *huu*, mnaona, kushuka pwani, na inanibidi kwenda mashariki.

115 Lakini alikwea kwenda Samaria, akasimama katika mji uitwao Sikari, kisha akawatuma wanafunzi Wake kwenda kununua chakula. Ndiposa walipokuwa wameingia katika mji wa Sikari, nini kilitokea? Yesu alikuwa ameketi kuegemea kilima, ndipo maskini mwanamke mmoja akatokea mjini. Hilo linapatikana katika Yohana Mtakatifu mlango wa 4. Mwanamke akatoka mjini, aitwaye mwanamke Msamaria. Sasa, sikilizeni kwa makini sana.

116 Mwanamke huyu akatokea. Sasa, alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya. Sasa, kama tungesema siku hizi, tungesema, "mwanamke malaya," au kitu fulani. Hili hapa tatizo lake, alikuwa na waume wengi kupita kiasi. Alikuwa amekuwa na waume watano, naye alikuwa akiishi na mmoja wakati huo, kwa hiyo hakuwa wake.

Kwa hivyo alitoka kwenda kuteka maji yapata saa tano, ndipo akaangalia pale akamwona Myahudi aliyesema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

117 "Mbona," akasema, "tuna," tuseme, "tuna ubaguzi hapa. Mbona, hupaswi kuniomba hayo, mimi ni Msamaria, na Wewe ni Myahudi. Hatuna uhusiano sisi kwa sisi."

118 Anafanya nini sasa? Sasa, hamna budi kuchukua neno langu, Yeye anawasiliana na roho yake. Baba alimwambia aende kule, lakini sasa huyu hapa ndiye mtu pekee ambaye Yeye alimwona, kwa hiyo akaja, hivyo huyo hana budi kuwa ndiye. Kwa hiyo anawasiliana na roho yake. Akasema . . .

Akasema, "Mbona, baba zetu walikinywea . . . "

Akasema . . . Kwanza, akasema, "Mimi . . . Kama ungeniomba Mimi, ningekupa maji usije hapa kuteka," akasema.

"Loo, kisima ni kirefu, Wewe huna kitu cha kuchotea."

Akaanza kuzungumza naye, mnaona, Yeye alikuwa akiishika roho yake.

Naye akasema, "Mbona, mnaabudia huko Yerusalemu; tunaabudia katika mlima huu," na kadhalika.

119 Akasema, "Saa inakuja ambapo waabudu halisi watamwabudu Baba katika kweli na roho." Akagundua shida yake ilikuwa nini, akasema, "Nenda, kamwite mume wako, mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Akasema, "Umesema kweli. Kwa maana umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

Mwangalieni maskini mwanamke huyo, alijua mengi juu ya Mungu kuliko nusu ya wahubiri wa siku hizi, katika hali yake. Akasimama, akashangaa sana.

Waangalieni . . . Waangalieni hao makuhani huko nyuma, walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli, mpiga ramli."

120 Lakini maskini mwanamke huyo kahaba alisimama, akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ndiwe *Yule* Nabii. Tunajua ajapo Masihi, atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe?"

Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye." Yesu jana.

121 Angalieni yale aliyofanya, aliacha huo mtungi wa maji, akakimbilia mjini, naye akawaambia watu hao, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?" Kwa maneno mengine, "Je, hii si ndiyo ile ishara ambayo Masihi ataonyesha?"

122 Angalia tofauti, wakati Nuru hiyo, huyo Roho, alipitia kwenye maskini hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani iliyolala pale . . . iliyokusudiwa Uzima wa Milele, hao walimu wa dini, haikuwasumbua hata kidogo. Waliwazia sana njia yao ya kufanya mambo, kwamba isingeweza . . . Ilibidi iwe njia yao, la sivyo hamna njia kabisa. Lakini wakati, ilipomgusa maskini kahaba huyo, alikuwa amekusudiwa Uzima. Akasema,

"Tunajua; tumefundishwa; tunaamini." Amina. "Tunajua ya kwamba ajapo Masihi, atatwambia mambo haya. U Nani Wewe?"

Akasema, "Mimi Ndiye."

123 Hilo lilitosha. Hilo lilikuwa ndilo. Huyu hapa aliona hiyo ishara ikifanywa, alijua ilikuwa ni Masihi. Alikimbilia mjini na kuwaambia watu, "Njoni, mwone Mtu huyu. Je, haimkini hii kuwa ndiyo ile ishara yenyewe ambayo Masihi anapaswa kufanya?" Mnaona? Nayo Biblia ilisema watu wa mji ule walimwamini kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke, haikumbidi kufanya jambo moja zaidi. Huyo mwanamke alishuhudia ni kweli, "Aliniambia nina waume watano, nanyi wanaume mnajua kuwa ninao." Ndivyo ilivyo. Naye alikuwa Masihi.

124 Sasa, kama hivyo ndivyo walivyomjua Yeye jana, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. . .Mnasema, "Na jana je?" Paulo alikuwa akiwaandikia Waebrania katika wakati wa Biblia. Jana, ilikuwa ni Mungu aliyekuwa ndani ya manabii. Je, mnaamini hilo? Mwangalieni Daudi, akipanda juu mlimani, mfalme aliyekataliwa, akilia, yapata miaka mia tano baada ya hapo, Mwana wa Daudi aliketi juu ya mlima ule ule, akilia, Mfalme aliyekataliwa.

125 Mwangalieni Yusufu, aliuzwa kwa vipande thelathini vya fedha, karibu vipande thelathini vya fedha. Mwangalieni. Alipozaliwa, alikuwa nabii. Angeweza kutabiri, kubashiri mambo yajayo, kutafsiri ndoto, wa kiroho, alipendwa na baba zake, akachukiwa . . . na baba yake na kuchukiwa na ndugu zake, jinsi Yesu alivyokuwa hasa. Mnaona? Na akatupwa shimoni na kudhaniwa kwamba amekufa, akatwaliwa na kuketi mkono wa kuume wa Farao. Hakuna mtu . . .

126 Gerezani mwake. . .Kama vile Yesu alivyotundikwa msalabani, gerezani Mwake, kulikuwa na mmoja aliyepotea, mmoja akaokolewa. Naye Yusufu, kulikuwa na mmoja aliyepotea, mmoja akaokolewa, ndipo akapanda karibu na Farao, wala hakuna mtu aliyeweza kuja kwa Farao, ila kwa njia ya Yusufu. Yesu alipaa juu Mbinguni, wala hakuna mtu ajaye kwa Baba, ila kwa njia ya Yesu. Na wakati Yusufu alipokiacha kiti cha enzi atoke nje, tarumbeta ililia, na kila goti likapigwa. "Pigeni goti! Yusufu yuaja." Naye Yesu atakapoondoka kwenye kiti cha enzi, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri. Mnaona? Huyo alikuwa ni Roho wa Masihi ndani ya watu hao. Hiyo ndiyo sababu Neno la Mungu liliwajia manabii. Na hapa Neno kamilifu la Mungu lilidhihirishwa ili kumkomboa mwanadamu.

Sasa, kama hicho ndicho alichokuwa jana, hicho ndicho alichokuwa leo. Kisha Paulo akasema Yeye atakuwa yule yule milele. Kwa hiyo tunaona.

127 Sasa, huyo hapo Myahudi na Msamaria wakija. Lakini sisi Mataifa, hatukuwa tunatazamia Masihi awaye yote, tulikuwa Warumi, na Waanglo-Sakson, tukiabudu sanamu, na kadhalika. Hatukuwa tukimtazamia Masihi awaye yote, kwa hiyo Yeye kamwe hakujionyesha. Hakuna hata wakati mmoja Yeye alifanya hivyo mbele ya Masihi, a-ha, mbele ya Mmataifa. Litafute katika Biblia, hakuna hata wakati mmoja. Kwa nini?

128 Sasa, kumbukeni, Yeye hawezi kubadilika. Ndipo mwishoni mwa kipindi cha wakati wa Wayahudi na hizo . . . Kama Yeye alithibitisha hilo kuwa ni Yeye Mwenyewe na kuwaacha Mataifa wapite, kwa theolojia tu, pasipo kuona jambo lile lile, basi Yeye si Mungu. Alifanya kitu fulani hapo . . . mwishoni mwa jamii yao, na wakati wao ambacho hakufanya hapa. Sasa, je, aliahidi jambo hilo? Naam. Upesi sasa, nami nitafunga.

129 Yesu alisema katika Luka Mtakatifu, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Mnajua hilo. Hebu tuangalie Sodoma, Ibrahimu, mfano wa Kanisa. Kumbukeni daima kuna matabaka matatu ya watu, hao ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Wako kwenye kila umati. Hawa hapa wanakuja.

130 Ibrahimu alikuwa amekuja muda mrefu, na kuona maajabu makuu mbele za Mungu, ishara kuu. Sasa, yeye anawakilisha Kanisa teule. Mungu alimpa Ibrahimu agano bila kuambatanishwa na masharti yoyote, akamwokoa katika neema Yake, ama, kwa neema Yake, bila masharti, kwa Ibrahimu na Uzao wake. Mnaona? Humtafuti Mungu, Mungu anakutafuta. Ulisema, "Nilitafuta na kutafuta." La, la. Ilikuwa ni Mungu akikutafuta, wewe usingejiachilia, hivyo tu. Unaona? Ni hayo tu. Mungu humtafuta mwanadamu, si mwanadamu kumtafuta Mungu.

131 Asili yenyewe ya mwanadamu ilionyesha katika bustani ya Edeni, alipotenda dhambi, badala ya kutoka na kuiungama, alikimbia. Haikuwa ni Adamu aliyekuwa akikimbia kwenye bustani akipiga kelele, "Mungu, Mungu, uko wapi?" Ilikuwa ni Mungu akisema, "Adamu, Adamu, uko wapi?" Mnaona? Jambo lile lile leo hii. Mnaona? Ni Mungu akimtafuta mwanadamu, "Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Mnaona?

132 Sasa, hawa hapa. Sasa, Ibrahimu alikuwa ameona mambo makuu mbele za Mungu. Sasa, Ibrahimu alikuwa na jamaa, mpwa, ambaye alikuwa ni Lutu. Naye Lutu alikuwa amechukua chaguo lake, huko chini akiishi kama ulimwengu, huko Sodoma. Mnajua hiyo hadithi? Kulikuwa na Wasodoma, wasioamini; kulikuwa na waaminio vuguvugu, Lutu na familia yake; huyu hapa Ibrahimu na familia yake, wameketi mahali *hapa*. Wakati ulikuwa umewadia wa Moto kushuka. Ilikuwaje? Sikilizeni kwa makini sasa katika kufunga.

133 Siku moja, kulikuwa na Malaika watatu waliokuja mbele ya kambi ya Ibrahimu, Mmoja wao alikuwa ni Mungu Mwenyewe. Ibrahimu akamwita, "Elohimu," ambaye ni Mungu, Bwana wangu, herufi kubwa B-w-a-n-a, Anayeishi peke Yake. Alikuja. . .Wawili kati yao walishuka wakaingia Sodoma, na kuihubiri Injili, na kujaribu kuwavuta watoke. Wote wanaoamini hilo semeni "Amina." Tunaamini hivyo. Lutu akatoka.

134 Unakumbuka jinsi Neno Lake lilivyokuwa kali? Hata Malaika alisema, "Hata usiangalie nyuma." Ndipo mke wa Lutu akageuka kutazama nyuma, kwa maana watoto wake na wajukuu walikuwa wakiteketea katika Hukumu za Mungu. Akageuka, naye angali amesimama pale hata wa leo. Huna budi kutii.

135 Mnasema, "Ni. . .loo, haileti tofauti yoyote yale. . . " Kweli inaleta tofauti. Maana mwanamke alikosa kuamini sehemu ndogo sana ya Neno, ikasababisha kila ugonjwa, huzuni, mauti, na chochote kile, ilikuwa ni Hawa.

136 Naye Yesu akasema, "Mkumbuke mke wa Lutu." Alikuwa na mengi zaidi ya kuangalia nyuma kuliko yale tuliyo nayo; watoto wake na wajukuu wake walikuwa wakiteketea katika Moto wa Hukumu ya Mungu, naye, huyo mama, akageuka tu kutazama nyuma, ila tu aliamriwa asifanye hivyo na huyo Malaika, naye akageuka hata hivyo, naye amesimama, leo hii, nguzo ya chumvi, fedheha, kote katika miaka.

137 Angalieni, sasa, Malaika hawa walikuja, na wawili miongoni mwao wakashuka na kumhubiria Lutu na familia yake. Hawakufanya miujiza mingi, walifanya miujiza michache, kama tu vile kuwapofusha macho wakati walipokuja kuwachukua. Nako kuihubiri Injili huyapofusha macho ya kafiri. Lakini walikuwa wakihubiri, "Ondokeni huku. Ondokeni Sodoma."

138 Lakini sikilizeni, Yule aliyekuwa akizungumza na Ibrahimu hakusema, "Ondokeni Sodoma," maana yeye na kundi lake hawakuwa Sodoma; hilo ni Kanisa teule. Sasa, kumbukeni, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Sasa, sikilizeni kwa makini.

139 Basi ni wangapi hapa ndani waliozaliwa mara ya pili? Hebu tuone mkono wako. Roho. . .Sawa. Mnapaswa kuwa na uwezo wa kula nyama sasa. Sikilizeni kwa makini. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Sasa, hawa wajumbe wawili, wajumbe mashuhuri, waliingia mle. Lutu alisema alitoa ujumbe wake, lakini haukusikika kuwa muhimu kwao. Hawakumjali hata kidogo, maana maisha aliyoishi yalithibitisha hilo, kanisa vuguvugu. Hata watoto wake mwenyewe hawakumwamini.

140 Lakini wakati wajumbe hawa walipoingia, waliona ya kwamba walikuwa ni watu watauwa. Na kama Sodoma haijawapokea watu wao watauwa siku hizi katika Oral Roberts na Billy Graham, kamwe sikumjua mmoja, watu watauwa, wakiwatikisa watoke.

141 Mwangalieni Billy Graham, yule mwinjilisti mashuhuri, huko nje Sodoma, akilipua, pasipo kufanya miujiza, lakini, "Ondokeni humu. Tubuni la sivyo mwangamie," analia. Basi sikilizeni, tumekuwa na watu mashuhuri kote katika nyakati, tumekuwa na Moody, Wesley, Sankey, Finney, Knox, Calvin, kote kote. Lakini kamwe hatukuwa na mjumbe, kwa kanisa hilo la kawaida, ambaye jina lake liliishia jinsi la Ibrahimu lilivyoishia, kuonyesha ya kwamba yeye alikuwa ni Mzao wa Ibrahimu, G-r-a-h-a-m kwa kanisa la kawaida. Tumekuwa na majina ya kila namna, lakini kamwe si jina hilo. Hili ndilo.

142 Na sasa, kulikuwa na Mjumbe aliyetumwa kwa Kanisa teule, Ibrahimu. Angalieni yale aliyofanya. Aliketi pale juu, Naye akasema, "Ibrahimu," sasa, kumbuka siku moja hapo kabla, jina lake lilikuwa Abramu, na jina la mkewe lilikuwa S-a-r-a-i, Sarai. Alilibadilisha likawa Sara, S-a-r-a, nalo jina lake Abramu likawa Ibrahimu.

143 Mwangalieni Mjumbe huyu sasa, anaonekana kama mwanadamu, amevaa nguo, mavumbi kwenye nguo Zake, ameketi, akila mbavu za ndama, na kunywa maziwa, na kula siagi, na mkate. Kweli. Ilikuwa ni Mungu ameketi pale. Naye akasema, "Ibrahimu, yuko wapi Sara, mkeo?" S-a-r-a. Alijuaje jina lake lilikuwa limebadilishwa kutoka kwa Abramu likawa Ibrahimu? Alijuaje alikuwa na mke? Naye alijuaje jina lake lilikuwa Sara?

Ibrahimu akasema, "Yuko hemani nyuma Yako." Angalieni, Biblia ilisema hasa *nyuma* Yake.

144 Angalieni hapa. Hapa inathibitika, "mimi," kiwakilishi nafsi, "Nitakurudia majira ya uhai, kama nilivyokuahidi." Mnaona alikuwa ni Nani? Ilikuwa ni Mungu aliyekuwa akizungumza naye wakati wote, kote safarini, kwa miaka ishirini na mitano aliyokuwa akimwamini. "Nitakurudia kulingana na. . . " Naye Sara, sasa, alikuwa na umri wa miaka tisini, na Ibrahimu alikuwa na mia moja. Ha—hawakuwa na maisha yoyote ya ndoa, kama mume na mke. Mnajua ninachosema, ninyi watu wazima. Mnaona, hiyo. . . wao. . . hayo yaliwaishia miaka mingi iliyopita, kwa sababu walikuwa wamezeeka sana.

145 Naye akacheka nafsini mwake akasema, [Ndugu Branham anaonyesha mfano—Mh.] tunachokiita huku—huku Marekani, alicheka kifichifichi, mwajua. "Mimi mwanamke mkongwe, na mume wangu anayeketi pale nje, mzee pia, basi tutakuwa na furaha tena, kama mume na mke wachanga?"

146 Ndipo Malaika huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema akasema: "Mbona Sara akacheka, akisema kwamba mambo haya hayawezekani?" Mnaona Kanisa hilo lilipata ishara ya aina gani? Walikuwa wamepata aina zingine zote za ishara, lakini hiyo ndiyo iliyokuwa ya mwisho.

147 Ndipo wakati uzao wa Ibrahimu, kupitia Isaka, uzao wa kimaumbile, Myahudi, ulipofikia mwisho wa maisha yao, huyu hapa Mungu yeye yule aliyedhihirishwa katika mwili, akionyesha ishara Yake ya Kimasihi, jambo lile lile. Sasa, hawa hapa Mataifa wanakuja, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, kupitia kwa Kristo, mwishoni mwa wakati wao, wakiwa na miaka elfu mbili ya mafundisho. Sasa, Wapentekoste walikuja na kunena kwa lugha, tafsiri, na kadhalika, nao walikuwa na miujiza ya kila namna. Lakini kumbukeni, sisi hapa, tuko kwenye mwisho wa wakati, tukipokea ishara ile ile waliyoipokea, kule nyuma, mwishoni mwa wakati, kabla tu ya Moto kushuka. "Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu." Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

148 Ungeangalia nini...? kwa maana huo Uhai uliokuwamo ndani ya Kristo ungekuwa katika Kanisa Lake. Mnaona? Mungu...Mtu huyo alikuwa ni Mungu, akajiwakilisha Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu, katika umbo la mwanadamu. Siku hizi, Mungu hujiwakilisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu wa Kanisa Lake. Mungu, Roho Mtakatifu, katika Kanisa Lake, akitenda kazi kupitia Kanisa Lake, akinena kwa lugha, akifasiri lugha, akiwaponya wagonjwa, na halafu ile ishara ya mwisho, Neno likidhihirishwa sana hata linakuwa, Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Ni wangapi wanaoona jambo hilo na kuamini hilo kuwa ni Kweli? Na tuombe.

149 Baba wa Mbinguni, mioyo yetu imejaa furaha, usiku wa leo, kujua kwamba Yesu angali hai. Miaka elfu mbili ya ukosoaji kamwe haiwezi kumbadilisha, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mipango ya elimu imejaribu kumbadilisha, madhehebu makubwa yamejitokeza, na kujaribu ku—kujaribu kulibadilisha, lakini Yeye ni Mungu asiyebadilika, habadiliki.

150 Siku moja, baada ya kufa, kuzikwa, na kufufuka Kwake, kulikuwa na marafiki wawili, wakienda zao barabarani, mioyo iliyofadhaika kwenye asubuhi ya Pasaka. Wakasema, wakinena juu ya kifo Chake na kuzikwa Kwake, "Angewezaje kuvumilia kufa?" huku akiwa Ndiye waliyedhania alikuwa. Ndipo Mtu akajitokeza vichakani na kuanza kuzungumza nao. Hawakujua alikuwa ni Nani. Lakini wakati wa jioni ulipofika, yapata wakati huu wa—wa jioni, wakamwomba aingie, kwenye nyumba ya wageni, na kukaa usiku kucha pamoja nao. "Ombeni nanyi mtapata." Wakafunga milango, na pale mezani, Yeye akafanya jambo fulani jinsi tu alivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwake, nao wakatambua kwamba hakuna mtu angeweza kufanya hivyo

kama Yeye. Kwa hiyo wakajua ilikuwa ni Yesu, Naye akatoweka machoni pao. Basi wakaenda mbio, na kuwaambia wanafunzi wale wengine, “Kweli, Bwana amefufuka!” Nao wakasema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?”

Tujalie tena, usiku wa leo, Baba. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

151 Nilikuwa nimeanza kuona watu wakiondoka, na bila kutambua . . . Wakati we—wenu wa usiku unakuja haraka sana hapa. Unaona? Huko chini nyumbani wa—wakati huu wa usiku, loo, imekuwa giza kwa saa kadhaa nyumbani, lakini hapa, ni . . . inaonekana kama tu unapojilaza kitandani, jua linateremka tu, inakubidi kuamka tena. Kwa hivyo ni . . . Samahani kwa kuwaweka muda mrefu sana.

152 Tutaitisha tu mstari mfupi wa maombi, usiku wa leo, na kuwaombea wagonjwa. Najua hii itakuwa mpya. Sasa, nitawaomba mfanye jambo fulani. Na hebu niseme, kama kila mtu ataendelea tu kuketi, kwa dakika kumi na tano tu zijazo, tutawashukuru. Mnaona?

153 Sasa, hawa Wahindi wanaoketi hapa, mbele, wamekuwa kwenye mikutano hapo awali, jana. Lakini nadhani wengi wenu ninyi wazungu hapa, na kadhalika, hamjawahi kuwa katika mojawapo ya hii mikutano. Lakini kumbukeni, Yeye anadumu yeye yule jana, leo, na hata milele. Na sasa, kama atakuja tu katikati yetu hapa, na kuonyesha ya kwamba Yeye ni yule yule . . .

154 Sasa, mavazi hayangeleta tofauti yoyote, ni Maisha, tendo, linalomfanya yule yule. Anatenda katika Kanisa Lake. Haijalishi jinsi anavyotenda kupitia kwangu, hana budi kutenda kupitia kwako, pia, kwa sababu sisi wawili tunakuwa kitengo Chake. Huna budi kuamini. Alipokuwa duniani, kulikuwa na miujiza mingi mikuu ambayo hangeweza kufanya kwa sababu ya kutokuamini kwa watu. Mnaona? Huna budi kumwamini, halafu basi kati ya hao wawili, kati yako na mimi, na wengine wakiamini, ndipo tunamwona Kristo akidhihirishwa kati yetu.

155 Sasa, upesi. Kwa kawaida, tunalifanya tofauti kidogo, lakini usiku wa leo, ninaamini ya kwamba Billy Paul aliniambia (Yuko wapi?), kwamba alisambaza ninii za maombi, ama, je, alisambaza kadi za maombi? Yeye hayupo hapa. Je, alisambaza kadi za maombi? Alisambaza? Vema. Angalieni huko nyuma, muone ni herufi ya aina gani. Je, ni A, B, C, au ni nini? [Mtu fulani anasema, “V.”—Mh.] Ati nini? [“V.”] V, V, sawa. Basi nadhani kwamba—kwamba mtu anaita . . . Ina—ina tano, ama sita, ama nane, ama kumi, ama kumi na tano, ama ishirini, ama thelathini, ama kitu kama hicho, kuna mtu yeyote aliye na mojawapo ya namba hizo? Sema tu, “Naam.” [“Naam.”] Vema. Basi, ni kutoka moja hadi hapo basi.

156 Hebu tuite kutoka namba moja basi. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Je, unaweza tu kuinua mkono wako? Mtu huyu hapa, njoo hapa, bwana. Namba mbili, kadi ya maombi namba mbili. Je, unaweza kuinua mkono wako, popote ulipo? Kadi ya maombi namba mbili. V, kama katika Victoria. V namba mbili, mbili katika V. V namba mbili. Vema. V namba tatu. Endapo huwezi kusimama, tutakukuita. Huyu mama hapa, sawa. Njoo huku, Mama. V namba nne. Ni nani aliye na hiyo? Namba nne. Je, unaweza kuinua mkono wako? Itatusaidia sana kama . . . Lo, samahani. Papa hapa. Namba tano. Vile tu sisi . . . Hiyo ni sawa, hiyo ni sawa. Namba sita. Kadi ya maombi namba sita. Sita. Je, kila mtu anazungumza Kiingereza? Ndugu Eddie yuko wapi? Kila mtu anazungumza Kiingereza? Mnaona? Sita.

157 Nilikuwa nje leo kwenye kaunta ya chakula cha mchana, na kuna kundi moja hapa linalozungumza lugha moja, moja hapa, lingine, huku mhudumu akizungumza lugha nyingine. Kwa hiyo na—najua kuna mchanganyiko wa lugha hapa. (Ati nini?) Sita? Saba. Hiyo ni sawa. Wakati mwingine wao ni viziwi wala hawawezi kusikia, kisha ninapokea barua ofisini ikisema, "Wao . . . Hakuna aliyeniambia, nilikuwa kiziwi." Saba, nane, nane? Sawa. Tisa, tisa, kadi ya maombi namba tisa. Mwangalie jirani yako, angalia kama ana kadi, inafanana na *hii*. Huenda ikawa yeye ni kiziwi sasa, au labda ni mlemavu, wala kamwe hawezi kusimama, mnaona, ama kitu kama hicho, basi itatubidi kuwabeba. Namba tisa.

158 Wana . . . Nimezungumza kirefu, na kuna watu kadhaa wametoka nje, labda ilikuwa. Sasa, watakosa namba yao. Namba kumi, yule mama pale. Namba kumi na moja? Kumi na moja? Loo, jamani, wataninii . . . [Mtu fulani anasema, "Huyo msichana mdogo."—Mh.] Loo, huyo msichana mdogo. Naam, namtakia heri! Namba kumi na mbili. Hapa. Namba kumi na tatu, kumi na tatu? Naweza . . . ? Hebu angalieni kote tena sasa, muone kama hakuna kiziwi au asiyeweza kusimama. Namba kumi na tatu. Hebu tukomee hapo.

159 Sasa, tafadhali, mnapopata kadi zenu, usichukue kadi, isipokuwa utakaa na . . . Maana inaninii . . . Sasa, kesho usiku, tutaita kutoka mahali pengine, mnaona, labda tuanzie hamsini, turudi nyuma, na ishirini, twende upande huo mwingine, ama kitu kama hicho. Mnaona? Mtaikosa kwa jumla, na hazibadilishanwi, lazima mziweke.

160 Sasa, huyu mvulana anakuja hapa alasiri moja, anazichukua kadi hapa mbele zenu nyote, na kuzichanganya zote pamoja, na kukupa tu kadi, mtu yeyote anayetaka moja, mpaka anasambaza idadi *fulani* yake. Lakini ni wangapi wanaojua ya kwamba watu wanaponywa zaidi huko kwenye kusanyiko, kuliko walioko jukwaani? Ni wangapi waliowahi kuwa katika mojawapo ya mikutano yetu hapo awali? Inua mkono wako. Loo, mko wengi kiasi. Naam, jamani! Kwa nini sikuchukua somo lingine usiku

wa leo basi? Mlijua kile. . . Mnaona? Jamani, sikujua kuwa nilikuwa miongoni mwao watu wa namna hiyo. Vema. Basi ninyi watu huko nje aminini kwa mioyo yenu yote.

161 Ni wangapi huko nje wasio na kadi ya maombi, na hata hivyo mnaamini Mungu atawaponya? Inua mkono wako, useme, "Naamini." Vema. Hebu niwaambie jambo fulani, yale Biblia isemayo sasa, Biblia ilisema ya kwamba wakati mmoja maskini mwanamke mmoja, tuseme, hakuwa na kadi ya maombi, lakini aliamini kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu, naye akasema, "Kama nikiweza tu kugusa upindo wa vazi Lake, nitaponywa." Ni wangapi wanakumbuka hiyo hadithi?

162 Naye alipomgusa. . . Mwanamke, alipomgusa, aligeuka, na akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Na wote. . . Mnaona, Yeye hakujua, Yesu asingeweza kusema uongo. Alisema, "Ni nani aliyenigusa?" Wala hakuna aliyejua. Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, Yeye akatazama huku na huku juu ya hilo kusanyiko. Imani yake, maana alihisi ndani yake ya kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma, imani yake ilikuwa imemponya. Asingeweza kushikilia, imani yake ilikuwa imefanya hivyo. Kwa hiyo imani yake katika Kristo, alimshika, na kumwambia ya kwamba imani yake ilikuwa imemwokoa. Hiyo ni kweli?

163 Sasa, sikilizeni kwa makini. Ikiwa Yeye ni sawa na alivyokuwa jana. . . Ni wangapi wanaoamini kwamba Biblia inasema kwamba Yeye sasa ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Vema, angetendaje kama ungemgusa? Sawasawa na alivyofanya wakati huo. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo ombeni sasa, ninyi msio na kadi za maombi, ama chochote kile, ombeni, na kuamini, na kusema, "Bwana Mungu, jalia nikuguse Wewe, na unene kupitia Ndugu Branham. Wewe ni Roho Mtakatifu; uko hapa. Nina imani Kwako, Ndugu Branham ana imani Kwako. Alitumwa hapa kutwambia tuninii. . . na kusema kwamba—kwamba ilikuwa. . . kuhusu kile Ukristo ulikuwa. Sasa, jalia. . . Nena kupitia kwake kama ulivyofanya, nami nitaliamini. Amina."

164 Sasa, vema. Sasa, iweni na kicho kabisa. Msijongee, tafadhalini. Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya Yesu Kristo. Sasa, kama ukiifuatilia hii mikutano popote pale, unajua kinachotokea, jambo fulani lingeweza kutokea vibaya sana. Mnajua, mmeliona likitukia. Mnaona? Kwa hiyo tulieni kabisa, na ujibu upesi tu, fanya lolote analokwambia ufanye sasa. Malaika wa Bwana yu karibu. "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

165 Sasa, je, yeyote wenu amewahi kuona ile picha ya yule Malaika waliyo nayo huko Washington, ile Nuru, yule Malaika wa Bwana? Wanayo hapa, nadhani, hawa watu wanayo hapa.

Sasa, kama Huyo ni Roho yeye yule hapa, kama alivyokuwa wakati huo, atalidhihirisha Neno, kama alivyofanya wakati huo. Hiyo ni kweli? Maana Huyo alikuwa ni Yesu huko nyikani, alikuwa ni Yesu alipofanyika mwili, alipofufuka alikuwa ni Yesu, aliporudi katika umbo la Roho Mtakatifu, alikuwa bado ni Yesu, yeye yule jana, leo, na hata milele.

166 Sasa, hakuna mtu humu jengoni ninayemjua. Siwajui wavulana hawa wanaoketi hapa, wao ni wavulana wa Kihindi kutoka hapa juu kwenye hifadhi, lakini mimi . . . walikuwa mkutanoni. Najua wa—wanatoka kule juu, lakini si—sijui majina yao. Na nje ya hao, kuna . . . na—najua kuna watu humu ndani . . . Nina baadhi ya . . . Ninaamini huyo ni baba yake Ndugu Borders, anayeketi papa hapa, na—nafikiri hiyo ni kweli, pale pale pembeni. Na—na huyo ni ndugu mwingine, ninasahau jina lake, na mke wake na mtoto mchanga, wanaoketi pale pale nyuma, lakini wanatoka hapa mahali fulani, nilikutana naye siku chache zilizopita. Na nje ya hao, sioni mtu yeyote humu ndani ambaye mimi . . . Ndugu Eddie, pamoja na mwanamume na mwanamke huyu, naam, wanaoketi papa hapa, walicheza muziki.

167 Kila mtu katika mstari huu wa maombi ambaye anajua sijui lolote kukuhusu, inua mkono wako, aliye kwenye mstari wa maombi hapa. Inua mikono yako juu, ikiwa wewe . . . ka—kama sijui lolote kukuhusu, inua mikono yako. Sawa. Wote huko nje, kwenye kusanyiko, wanaojua sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu. Sawa. Haya basi.

168 Sasa, huyu hapa mtu amesimama, kwa mara yetu ya kwanza kukutana. Sininii . . . Loo, huenda alikuwa mkutanoni mahali fulani, ama kitu kama hicho, lakini namaanisha, kumjua, simjui. Mungu anamjua, simjui, lakini hapa tunakutana kwa mara ya kwanza. Sasa, sijui uko hapa kwa sababu ya nini . . . Je, mnaweza kunisikia, kote kwenye kusanyiko? Mnaona? Sawa. Sasa, sikilizeni kwa makini sana.

169 Sasa, sijui kwamba Kristo atafanya jambo hilo, lakini kama akilifanya, basi hilo linaonyesha ya kwamba "sisi tunataka kumwona Yesu." Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ukristo, nilisema muda mfupi uliopita, ulikuwa unashawishi unapofundishwa kwa urahisi wa Neno, na kisha uishiwe jinsi upasavyo kuishiwa, kama vile Kristo, sio Mkristo, Kristo katika mwaminio Mkristo.

170 Sasa, kama ulikuwa hapa kwa ajili ya matatizo ya kifedha, sasa ningeninii . . . ningekuwa wa msaada kidogo sana kwako. Ikiwa uko hapa kwa matatizo ya nyumbani, nisingejua jinsi ya kupata wakati wa kuongea nawe pamoja na mke wako, endapo unaye. Kama uko hapa kwa ajili ya ugonjwa, hakuna kitu ningaliweza kufanya juu yake, ni kukuwekea tu mikono. Lakini vipi kama wewe, tuseme, ulikuwa hapa kwa sababu ya ugonjwa,

nami nije, nawe, tuseme, ulikuwa na kansa, nami nikajitokeza, nikasema, "Bwana, una shida gani?"

Ungesema, "Nina kansa, bwana."

171 "Utukufu kwa Mungu. Yesu alisema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa,' Haleluya! 'watapata afya.' Bwana abarikiwe, endeleeni mbele." Naam, hiyo inaweza kuwa kweli. Mnaona? Huo unaweza kuwa ni ukweli. Unaona? Hatuna la kusema dhidi ya huo. Lakini sasa, vipi . . . Ungekuwa na . . . ungeshangaa kama . . . juu ya hilo, Ndugu.

172 Lakini sasa, vipi kama Kristo akija na kukwambia vile umekuwa, ama jambo ambalo umefanya, ama akwambie shida yako ni nini, ama jambo fulani, kama Yeye alivyofanya katika Biblia, niliyozungumzia, usiku wa leo? Basi ungejua hayo yalibidi yatoke kwa nguvu za kimbinguni. Hiyo ni kweli? Kusanyiko lingeamini hilo? Halina budi kupitia kwa mambo ya kimbinguni, kwa maana hii hapa Biblia juu ya moyo wangu, kadiri nilivyopata kumwona huyu mtu, Mungu Mbinguni anajua sijawahi kumwona, nijuavyo mimi, isipokuwa iwe nilimpita mtaani, ama aliketi mkutanoni mahali fulani, ama kitu kama hicho, bali kumjua, simjui. Hiyo ni kweli.

173 Sisi hapa tumesimama. Sasa, Roho Mtakatifu akinifunulia shida yako, ama jambo fulani kuihusu, basi tutajua kwamba tumemwona Kristo yeye yule. Sasa, unajua itabidi ziwe ni nguvu za kimbinguni. Ninyi nyote mnajua hilo. Baadhi yenu mngeweza kusema, "Vema, si ya Mungu." Vema, hivyo ndivyo Mafarisayo walivyosema, mna thawabu ya namna hiyo. Kama ni Mungu, mmemkufuru Roho Mtakatifu, wala hakuna msamaha kwa jambo hilo. Mnaona? Sasa, kama unaamini ni Mungu, basi unapokea thawabu ya Mungu. Kumbuka, si mimi, ni Yeye. Unaona? Yeye, Kristo.

174 Naam, bwana. Mnaweza kuona, hiyo hapo Nuru hiyo imemzunguka, sasa hivi. Anafahamu hilo, hisia tamu na nzuri kweli imekuzunguka. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mnaona? Mnaona? Hiyo ni kweli. Hivi huwezi kuiona hiyo Nuru? Zumaridi? Huyu hapa. Amekuwa chini ya mateso haya kwa muda mrefu, ni fadhaa. Umekuwa katika matatizo mengi sana, hata hujaweza kufanya kazi kwa muda mrefu, sikuzote unaugua.

175 Mimi . . . Kila mkutano napata mtu ambaye hatajali. Kwa nini mnashuku? Mtu fulani alisema, "Alibahatisha hayo." Sikubahatisha.

176 Simoni Petro alipokuja kwa Bwana wetu, alimwambia alikuwa ni nani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia u nani wewe? Je, ingekufanya utambue kwamba nimekwambia ukweli basi, kwamba fadhaa yako imekwisha? [Ndugu huyo anasema, "Ninatambua."—Mh.] Unatambua? ["Ninatambua."] Bw. Ripping, nenda, amini kwa moyo wako wote na upone.

Unamwamini? Unamwamini Kristo? Sasa, sasa, mwulizeni. Ikiwa mnamjua mtu huyo, mwulizeni.

177 Iweni na kicho kabisa. Tafadhalini, msitembee-tembee. Unaona, wewe ni roho, na unapojongea iko chini ya mawasiliano, nayo inaendelea tu kunivuta. Ketini tu hapo na kuamini, iweni na imani. Tumieni tu dakika zingine chache.

178 U hali gani, mama? Hatufahamiani. Sisi ni, naam, nadhani wewe ni mzee kidogo kuliko mimi, na labda tumeachana kwa miaka kadhaa, na maili kadhaa. Sisi hapa tunakutana kwa mara ya kwanza, kama vile Bwana wetu alivyokutana na mwanamke mmoja, wakati mmoja, kisimani, Yohana Mtakatifu 4, Sikari. Ndipo akazungumza naye muda mrefu kutosha kujua shida yake ilikuwa nini, na kumwambia shida yake ilikuwa nini, naye akaamini. Naye akaenda na kusema, "Njoni, mwone Mtu, aliyeniambia shida yangu ni nini. Haimkini Huyo kuwa ndiye Masihi?" Je, unaweza kuamini jambo lile lile, mimi na wewe tukikutana pamoja? Je, kila mwanamke hapa ndani angeamini jambo lile lile?

179 Huu hapa mkono wangu kwenye Biblia, sijawahi kumwona mwanamke huyu, sijui lolote kumhusu, lakini huyu hapa amesimama, anaonekana kama mtu mzuri. Naam, huyu mama anaugua, jambo moja, ninamwona akijaribu kutoka kitandani, ni yabisi-kavu, ana yabisi-kavu. Halafu basi jambo lingine, unasikia kwa shida, husikii vizuri sana. Hiyo ni kweli. Kitu kingine, una tatizo la uso wako, naona umefanyiwa upasuaji. Mumeo huko nje ni mgonjwa pia. Hiyo ni kweli. Unaamini sasa Yeye atakuponya? Vema. Nenda, amini, nawe utapokea ulichoomba, katika Jina la Bwana Yesu.

Unaamini? Amini. Usitie shaka. Amini kwa yote yaliyo ndani yako sasa. "Kama unaweza kuamini . . . "

180 U hali gani? Hunifahamu, sikufahamu, Kristo anatujua sote wawili. Kwa kudhania, nikikutazama, wewe ni Mhindi, wewe ni Mhindi. Sawa. Sasa, sisi hapa tunakutana kama . . . Hii hapa— hii hapa ni Yohana Mtakatifu 4 hasa. Huyu hapa mwanamume mzungu na mwanamke wa Kihindi, wakikutana hapa, kama vile Yesu, akiwa Myahudi, na mwanamke Msamaria. Alimjulisha, upesi sana, ya kwamba Mungu alikuwa Mungu wa jamii zote, na hiyo ni kweli.

181 Sasa, kama Mungu atanifunulia yaliyo moyoni mwako, ama jambo fulani kukuhusu, utajua kama ni kweli, au la. Je, utamkubali na kumwamini kwa moyo wako wote, na kuamini ya kwamba Yeye ndiye Masihi aliyefufuka, na anayefanya hivi ni Roho Wake? Utaamini? Mungu na akujalie haja yako. Ninaona mtoto, ni mtoto mchanga. Unamwombea mtoto, mtoto wako, yuko hospitalini. Basi unaamini Mungu anaweza kuniambia kile huyu . . . tatizo la huyu mtoto mchanga? Ana ugonjwa wa moyo, nawe unaomba kwamba Mungu atamhurumia. Usitie shaka,

Mungu anakupa haja yako. Nenda sasa, na umwache mtoto wako apone. Sasa, usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote.

Je, unaamini? Amini. Usitie shaka. Hatufahamiani; Bwana Mungu anatujua sisi sote wawili hata hivyo.

182 Alifanya jambo fulani kwenye kusanyiko, nami sikulipata wakati huo, mtu fulani akiomba. Kuwa tu na imani, usiwe na shaka. Amini kwa moyo wako wote, maana Yeye ni Mungu, hawezi kushindwa.

183 Angalia hapa, kwa dakika moja tu. Kwa kuwa. . .Kama ningeweza kukusaidia wala nisifanye hivyo, basi singefaa kusimama nyuma ya mimbara, hapa, na Biblia. Huo ugonjwa wa tezi dume unakuacha. Amini kwa moyo wako wote, Mungu anakuponya. Uligusa nini? Upindo wa vazi Lake. Unaona? Amini. Yeye si ni wa ajabu?

184 Yabisi kavu, mwanamume, ameketi, akiniangalia, amevaa miwani, kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakupa afya. Unaamini? Unakubali? Mungu akubariki. Je, una kadi ya maombi? Huhitaji moja, imani yako inakufanya mzima. Amina.

185 Aligusa nini? Mnaona, alikuwa ameketi pale akiomba, naye akamgusa Kuhani Mkuu, Kuhani Mkuu akaligeukia Kanisa Lake na kuzungumza. "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Je, hamwoni kwamba Yeye yu hai? Hatumtumikii Mungu aliyekufa, Yeye ni Mungu aliye hai. Huyo Ndiye. Huo ni Uwepo Wake, yale aliyoahidi papa hapa, Kanisa likipata ishara Yake ya mwisho, kabla tu ya Moto kushuka sasa. Iweni tu na imani, msitie shaka.

186 Sasa, huyu hapa maskini mama mmoja, simjui, sijawahi kumwona, sisi ni wageni kabisa. Lakini ikiwa Bwana Mungu atanifunulia jambo fulani kuhusu huyo mwanamke, je, itawafanya ninyi nyote kuamini, na mtajua Yeye yuko hapa? Mtaamini kwa moyo wenu wote?

187 Bila kukujua, lakini hata hivyo Mungu anakujua, na Mbele Zake, tunaposimama, wewe ni Mkristo, nawe unaugua udhaifu fulani, kitu kama ugonjwa wa moyo. Hapa, ni moyo dhaifu tu. Kuna kitu cha kigeni kukuhusu, hata hivyo, naona maji yanayotiririka. Unaona? Wewe ni mmishenari, na unajaribu kupata nguvu kurudi mahali fulani, ni—ni—ni Brazil. Amini kwa moyo wako wote, nawe unaweza kurudi na kuihubiri Injili, na kuwa mmishenari.

188 Unaamini kwa moyo wako wote? Kamwe usitie shaka, bali amini, kwa moyo wako wote, ya kwamba Bwana Mungu wetu na Baba wa Mbinguni yuko hapa. Vipi kama hata sikukuambia chochote, nilikuwekea tu mikono. Ungeamini ungepona? Je, ungeamini? Uliamini papo hapo. Vema, u—uliponywa, ulipoketi kwenye kiti chako, uliposimama. Hisia hiyo ya kigeni kweli ilikuja juu yako. Niliona ulichukua mahali pako kwenye mstari wa maombi. Imekwisha. Nenda. Mungu akubariki.

Njoo. Aliposimama, hiyo Nuru ilimpiga huyo mwanamke, ndiyo sababu nikasema mara moja, huyu hapa Malaika wa Bwana.

189 U hali gani? Je, unaamini Mungu huponya ugonjwa wa moyo, anawaponya watu? Aliuponya moyo wako, pia. Kwa hivyo pita tu uende, ukisema, “Asante, Bwana,” na uamini, kwa moyo wako wote, naye Mungu atakuponya.

190 U hali gani? Unaniamini mimi kuwa nabii Wake, mtumishi Wake? Unaaamini? Mungu huponya yabisi kavu pia, sivyo? Anakupa afya pia. Unaamini? Sawa. Endelea, yabisi kavu yako itakuacha. Mwamini Mungu.

191 Ulitoa miwani yako kabla hujafika hapa. Vema. Lakini hilo silo jambo kuu. Je, unataka kwenda kula chakula chako cha jioni, na maskini ugonjwa huo wa tumbo utaondoka, nawe upate afya? Nenda ukale, Yesu Kristo anakuponya. Amini sasa, kwa moyo wako wote.

192 Mwanamke huyu ni mwanamke mwenye fadhaa, ana wasiwasi mwingi sana, na imefikia mahali ambapo tumbo lake linamsumbua kutokana nao, ni tumbo lenye fadhaa, ugonjwa wa mmeng’enyo tu—tumboni. Unaamini kwamba unaweza kwenda ule sasa? Unaukubali, na kuamini? Vema. Nenda ukaamini basi, katika Jina . . . Sasa angalia, kweli sio tumbo lako, ni mishipa yako. Kwa hiyo inakupasa tu kushikilia imani, na kuendelea huko nje, na uwe mzima. Yesu Kristo atakuponya, ukiamini.

193 Vema. Mlete huyo msichana mdogo. U hali gani? Wewe ni msichana mdogo anayependeza. Je, unaamini ya kwamba Yesu alipokuwa hapa aliwachukua wasichana wadogo, kama wewe, na kuweka mikono Yake juu yao? Na kama walikuwa na maskini uvimbe huo puani, mbaya kadiri ulivyo nao, je, unaamini wangepona? Je, unaamini Yeye alinituma, nikakuwekee mikono yangu? Vema, wewe inama. Baba wa Mbinguni, ninamhukumu ibilisi huyo anayemsumbua mtoto huyu, na umwache, ugonjwa huu wa pumu, wala usirudi tena. Katika Jina la Yesu. Amina. Nenda, sasa, kipenzi, utapona, na umwamini Mungu kwa moyo wako wote.

194 Njoo huku, dada. U hali gani? Hatufahamiani, lakini Mungu anatujua sote wawili. Je, hiyo ni kweli? Sasa, wanawake wa takriban umri wako kwa kawaida wana ugonjwa wa fadhaa kwa vyovyote vile. Umekuwa nao kwa muda mrefu kiasi, nao umekuacha na tumbo baya, huwezi kula. Nakuona ukiondoka mezani, ukiacha vitu ambavyo . . . lakini haikubidi kufanya hivyo tena sasa. Anakuponya. Nenda ukale. Amini kwa moyo wako wote, katika Jina la Bwana Yesu.

195 Je, mnaamini kwa moyo wenu wote, huko nje? Kama mnaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Mwanamume anayeketi hapa, kando ya mama mmoja, akinitazama, sasa, moja kwa moja, ugonjwa wa tezi dume, fadhaa, akiamka usiku,

ulifikiri Yeye angekosea, lakini hakukosea. Ulikuwa ukiombea jambo hilo. Inua mkono wako, kama hivyo ndivyo. Mungu akubariki. Yote yamekwisha sasa, nenda nyumbani, pumzika vizuri usiku wa leo. Yesu Kristo anakuponya.

196 "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Je, mnamwamini? Je, kuna waaminio wangapi humu jengoni? Inua mkono wako. Yesu alisema hivi pia: "Ishara hizi zitafuatana na waaminio." Hiyo ni kweli? "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hivyo ndivyo alivyosema? Vema, kama Yeye yuko hapa sasa, nanyi mnaona ya kwamba Yeye yuko hapa, je, hatakutimizia Neno Lake? Basi wekeaneni mikono; wekeaneni tu mikono. Vema. Hiyo ni sawa. Wekeaneni mikono, ninyi mnaotaka kuamini.

197 Sasa, kama wewe ni mwaminio, mwombee mtu huyo uliyemwekea mikono yako. Naam, bwana, na hiyo TB, usiijali tena, imekwisha, amini. Rudi kwenye hifadhi yako ukimsifu Mungu, yote yamekwisha. Ninakusahi uamini. Yesu Kristo yu hai usiku wa leo; Yuko hapa, miongoni mwetu, sasa hivi. Mwo—mwombee mtu huyo uliyemwekea mikono yako, maana wanakuombea. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

198 Baba yetu wa Mbinguni, tumebarikiwa sana, usiku wa leo, kumwona Roho Mtakatifu mkuu akitujia hapa, kwenye kisiwa hiki, usiku wa leo na kujidhihirisha Mwenyewe kama Bwana aliyefufuka, yeye yule jana, leo, na hata milele. Waaminio wameketi hapa, wamewekeana mikono; wanaombeana huku Uwepo Wako ukiwa hapa.

199 Ee Mungu, hivi watu wanaweza kufa ganzi sana katika roho hata wasiweze kutambua Uwepo Wako? Ndipo tunajua, Bwana, wamepotea Milele. Lakini, Baba, watu hawa hapa wanaoamini ya kwamba Wewe uko hapa na wako tayari kukupokea, wamewekeana mikono. Nimedhoofika, nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utatuma thibitisho la imani moyoni mwao, kumpokea Kristo, yule Mponyaji mkuu, ndani ya mioyo yao wakati Yeye yupo. Lijalie.

200 Na Shetani, wewe uliyewafunga kwa maradhi na magonjwa haya, nakushutumu. Wewe ni kiumbe kilichoshindwa, umefichuliwa hapa. Watu ambao wamekusikiliza wanajua, usiku wa leo, ya kwamba umefichuliwa, wala huwezi kuwashikilia tena. Unasema uongo tu, nasi tunachukua mamlaka kwa kusema kwamba tunasimama katika Jina la Yesu Kristo, Ambaye alifufuka kutoka kaburini, na kwa Damu Yake na Uzima Wake alikushinda na kukuvua kila mamlaka uliyokuwa nayo. Huna mamlaka, wewe ni mwongo, nasi tunakuita uwaache watu hawa. Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yao wapate kuwa wazima!

201 Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, naye Mungu atawainua. Kama wewe ni mwaminio halisi, nawe

unaamini ya kwamba uko Mbele za Kristo, na unataka kukubali uponyaji wako, sijali umelemaa jinsi gani, kwamba shida yako ni nini, simama kwa miguu yako katika imani, ukiamini na Yesu Kristo atakuponya. Simama, haijalishi una tatizo gani, simama kwa vyovyote vile, kama unaamini. Amina. Hilo hapo kusanyiko zima limesimama. Huyu hapa, Roho Mtakatifu mkuu akitembea kati yenu. "Na—nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Hebu tuinue mikono yetu, na tumpe sifa sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza

Mnampenda? Inueni mikono yenu, na kumsifu, na kumwambia kwamba mnampenda.

202 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa wema Wako, kwa fadhili Zako, kwa rehema Zako, kwa imani ya watu hawa. Mungu, pitia kwenye mji huu mkubwa. Kutoka nje hapa, tunaomba watu watafanya hivyo, Bwana, na kuwaleta wagonjwa, vipofu, vilema, viwete, na wanaoteseka, na jalia nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini zije mbele na kukithibitishia kisiwa hiki, kabla haijachelewa kupita kiasi, ya kwamba Yesu Kristo yu hai, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

203 Sasa, mpeni sifa. Inueni mikono yenu na kumsifu, na Mungu awe pamoja nanyi hata tutakapokutana. Vema.

62-0727 Sisi Tunataka Kumwona Yesu
Curling Arena
Victoria, British Columbia Canada

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org